

SIO SIRI

KAMATI YA BARAZA LA SENETI INAYOSHUGHULIKIA MAJESHI

TAARIFA YA

GENARALI WILLIAM E. WARD,

KAMANDA MAREKANI



KIKOSI MAALUMU CHA JESHI LA MAREKANI AFRIKA

MBELE YA KAMATI YA BARAZA LA SENETI INAYOSHUGHULIKIA MAJESHI

Machi 9 2010

KAMATI YA BARAZA LA SENETI INAYOSHUGHULIKIA MAJESHI

www.africom.mil

SIO SIRI

KAMATI YA BARAZA LA SENETI INAYOSHUGHULIKIA MAJESHI – MUHTASARI WA TAARIFA KWA MAANDISHI

UTANGULIZI

MAZINGIRA KIMKAKATI

- Asili ya Mazingira
- Maeneo yenyewe Uwezekano wa kutokea Mgogoro na Athari kwa Amani na Ulinzi
- Changamoto Kimataifa – Siasa Kali ya Utumiaji Nguvu, Usafirishaji Haramu, Uharamia
- Afya ya Umma, Maendeleo ya Kiuchumi, na kuleta Demokrasia Sekta ya Ulinzi ya Afrika

MTAZAMO WA KIKOSI MAALUMU CHA JESHI LA MAREKANI AFRIKA

MIPANGO YA KIKOSI MAALUMU CHA AFRIKA NA SHUGHULI ZAKE

- Kujenga Uwezo wa Majeshi ya Kawaida ya Washirika
- Kusaidia Kujenga Uwezo wa Majeshi ya Ulinzi ya Washirika
- Kujenga Uwezo wa Utendaji wa Majeshi Washirika
- Kudumisha Uhusiano Mkubwa wa Mikakati
- Kutekeleza Mabadiliko katika Sekta ya Ulinzi wa Kujitetea
- Kuleta Ushirikiano wa Maeneo, Hali ya Kujitambuwa, na Utendaji
- Kupambana na vitisho vya Kimataifa na Siasa Kali
- Kuchangia Ushwari katika Maeneo ya Sasa yenyewe Migogoro
- Kukabiliana na Hali ambazo Zinachangia Kutokuwepo Ushwari

VIJENZI SAIDIZI KWA SHUGHULI ZA KIKOSI MAALUMU

- Jeshi la Nchi Kavu la Marekani, Afrika (USARAF)
- Jeshi la Majini la Marekani, Afrika (NAVAF)
- Jeshi la Angani la Marekani, Afrika (AFAFRICA)
- Jeshi la Marine la Marekani, Afrika (MARFORAF)
- Jeshi la Operesheni Maalumu , Afrika (SOCIAFRICA)
- Kikosi Mchangamano cha Majukumu ya Pamoja – Pembe ya Afrika (CJTF-HOA)

UWEZESHAJI WA KIKOSI MAALUMU: CHANGAMOTO NA FURSA

- Mamlaka
- Miundombinu katika Uwanja wa Shughuli na Mahitaji ya Hali
- Uwezo
- Uunganishaji wa Shughuli na Michango ya Idara Mbali Mbali
- Mipango ya Mafao

HITIMISHO

UTANGULIZI

Ni heshima kubwa kwangu kama kamanda wa Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kutowa Taarifa ya hali halisi kwa mwaka huu wa 2010. Operesheni za Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika na mipango yake hulinda maisha ya raia wa Marekani na masilahi ya Marekani katika Afrika na ndani ya Marekani, kwa kuunga mkono ulinzi na ushwari katika Afrika na katika visiwa vya bara hilo. Sisi tunazingatia mkakati wetu na juhudzi zetu katika kuzisaidia nchi za Afrika kujenga majeshi yenyewe uwezo na yenyewe kitaalamu ambayo yanakuwa chini ya mamlaka ya kiraia, majeshi yenyewe kuheshimu haki za binadamu na yenyewe kutii sheria za nchi. Sisi tunawasaidia washirika wetu wa Afrika katika kujenga uwezo wa kupambana na vitisho vya kimataifa kutoka mashirika yenyewe siasa kali yenyewe kutumia nguvu; kuzuia biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, dawa za kulevyo, na silaha; kusaidia katika operesheni za kulinda amani; na kukabiliana na athari za maafa ya kibinadamu – yawe yamesababishwa na binadamu au ya asili – ambayo yanababishwa upotevu wa maisha ya watu na kuwaacha watu bila masikani.

Usaidizi wa ujenzi wa majeshi ya kitaalamu na yenyewe uwezo unachangia katika kuongeza ulinzi na ushwari katika Afrika – na kuziruhusu nchi za Afrika na mashirika ya maeneo ya Afrika kuhimiza demokrasia, kupanuwa maendeleo, kutowa uwezo kwa ulinzi wao wa kujitetea, na uwezo wa kuwatumikia vyema watu wao.

Katika hotuba yake nchini Ghana mwezi Julai mwaka jana, rais Obama alithibitisha tena umuhimu wa kimkakati wa bara la Afrika kwa Marekani na kwa maslahi ya taifa letu. Alitambulisha mahitaji manne muhimu katika juhudzi za serikali ya Marekani za kujihusisha katika bara la Afrika:

- Kuunga mkono demokrasia zenyewe nguvu na zenyewe kuendelea pamoja na utawala bora
- Kuleta maendeleo ya kiuchumi na maendeleo ya jumla yenyewe kuijendezea
- Kuongeza upatikanaji wa huduma bora za afya na elimu
- Kusaidia kuzuia, kupunguza, na kutatuwa migogoro yenyewe kutumia silaha

Kwa kupitia shughuli za ulinzi zenyewe kuendelezwa pamoja na majeshi ya Afrika, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinaunga mkono malengo ya taifa la Marekani na malengo ya rais wa Marekani na yale ya washirika wetu wa Afrika – hivi sasa na huko mbele.

Katika ripoti hii, ninatowa maelezo ya jumla kuhusu hali ya kimkakati katika bara la Afrika, tunaelezea mwelekeo wetu wa kimkakati, na kuonyesha jinsi gani juhudzi zetu za ushirikiano wa ulinzi, ambao umepangwa na kutekelezwa kwa ushirikiano wa karibu sana na

washirika wetu wa idara mbali mbali, zinavyoleta ushwari katika Afrika zikiunga mkono sera za mambo ya nchi za nje za Marekani na malengo ya ulinzi wa taifa.

HALI YA MAZINGIRA KIMKAKATI

Changamoto na fursa kwa Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani katika Afrika katika Upande wa Majukumu (AOR) ni ngumu na mzito. Uhusishwaji wa jeshi peke yake una maana hautoshi kuwasaidia washirika wetu kukabiliana nazo. Kikosi cha Jeshi Maalumu la Marekani katika Afrika kinataka kuwa sehemu ya juhudini zenyenye kushirikishwa ambazo zinaunganisha vyombo vyote vilivyopo katika mataifa yetu washirika na katika idara mbali mbali za washirika wetu.

Mjadala wetu kuhusu hali ya mazingira kimkakati katika Afrika unaanza na swala muhimu la wasi wasi katika Wizara ya Ulinzi ambao ulielezewa na Rais: uwezekano wa kutokea migogoro, vitisho vya kimataifa, na vitisho vingine dhidi ya amani na ulinzi. Unafuatiwa na maelezo kuhusu maswala muhimu ambayo yanakabili majeshi ya washirika wetu Afrika wakati wanapotaka kukabiliana na vitisho hivi.

Hali ya Mazingira

Afrika ni bara kubwa lenye anuwai tofauti ambapo maeneo ya ardhi ni kiasi cha mara tatu na nusu cha taifa la Marekani. Umbali kutoka eneo la kaskazini kabisa ya bara la Afrika hadi eneo la kusini kabisa la bara hilo ni sawa hivi na umbali kutoka New York hadi Moscow. Nchi 53 za bara hilo zina historia zake za kipekee.

Afrika ni nyumbani kwa watu bilioni moja, wakigawanyika katika makundi 800 ya kitamaduni na mila na wakizungumza lugha 1,000 tofauti. Uhusiano wa kikabila na kitamaduni mara nyingi unashawishi mwelekeo wa siasa za taifa. Mwongezeko wa idadi ya watu katika Afrika kiwango chake ni cha juu duniani. Miongoni mwa nchi 40 duniani kote zenyenye kiwango kikubwa cha mwongezeko wa idadi ya watu, nchi 34 zipo katika bara la Afrika.

Wakati nchi zenyenye kuongezeka katika Afrika zinafanya uchaguzi, mahitaji mengi zenyenye kuhitajika kuendeleza demokrasia, kama vile utiifu wa sheria, ulinzi wa haki za mtu binafsi, na udumishaji wa haki za jamii, ni mambo ambayo yanaanza kuwepo au hayapo kabisa. Zaidi ya hivyo, katika baadhi ya nchi ambazo zilionyesha kuwepo kwa demokrasia na uhuru huko nyuma, zinatokeza na muongezeko wa utawala wa mfumo wa mabavu.

Maeneo zenyenye Uwezekano wa Kutokea Migogoro na Athari kwa Amani na Ulinzi

Afrika bado inakabiliana na athari za kuenea kwa migogoro ambayo ililikabili bara hilo kufuatia harakati za vyama vilivyogombea uhuru katika nusu ya mwisho ya karne iliyopita, na baadhi ya harakati hizo zinaendelea bado hii leo.

Athari za migogoro yenye kutumia silaha katika Afrika ni kubwa mno. Umoja wa Afrika (AU) unakadiria kwamba Afrika ina idadi kubwa sana duniani ya watu amba wamepoteza masikani yao kutokana na utumiaji nguvu, kukiwepo karibu na watu milioni tatu amba ni wakimbizi na kiasi cha watu milioni 11.6 amba wamepoteza masikani yao ndani ya nchi 19 katika bara zima.

Kufuatana na utafiti uliofanywa mwaka 2007 na shirika la kimataifa la Oxfam juu ya athari za kiuchumi zenye kutokana na migogoro ya utumiaji wa silaha, nchi 23 za Afrika zilipoteza kiasi cha dola za Kimarekani \$284 za mapato yake kati ya mwaka 1990 na 2005 kutokana na migogoro yenye kutumia silaha. Oxfam ilikadiria kwamba mgogoro wenye kutumia silaha katika Afrika unaathiri uchumi kwa kiasi cha asilimia 15 kwa wastani. Migogoro ni kizuizi kikuu kwa maendeleo na utowaji wa huduma za msingi kwa jamii, kama vile huduma za afya na elimu.

Hii leo, operesheni nane miongoni mwa operesheni 17 za kulinda amani zenye kuendelea au tume za kisiasa zenye kuendeshwa na Umoja wa Mataifa (UN) zipo katika bara la Afrika. Tume nane katika Afrika zimechukuwa asilimia 75 ya walinda amani wa Umoja wa Mataifa, wanajeshi, polisi na maafisa wa kiraia duniani kote. Idadi na kiwango cha tume za kulinda amani zinaleta mzigo mkubwa kwa mataifa yenye kutowa misaada pamoja na mashirika ya kimataifa. Kwa hiyo, ni kwa masilahi yetu kuwasaidia washirika wetu wa Afrika kuimarisha jitihada zao na kuongeza uwezo wao.

Wakati idadi ya migogo yenye kutumia nguvu katika Afrika imepunguwa katika miaka 10 iliyopita, uwezekano mkubwa wa kutokea migogoro mipya na kuendelea kwa migogoro bado upo.

- Nchini Sudan, eneo la Dafur bado halina usalama, utumiaji nguvu umeongezeka kusini mwa Sudan, na hali ya wasi wasi inaendelea katika maeneo ya mpaka.
- Somalia inabakia kuwa nchi iliyomo katika mgogoro wenye kutumia silaha, wakati serikali kuu ya mpito (TFG) inapigana vita dhidi ya utumiaji nguvu wenye kufanywa na Waislamu wenye siasa kali.
- Licha ya mbano wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi la Uganda (UPDF), bado makundi yaliyotawanyika ya wapiganaji wa Lord Resistance Army yanaendelea na shughuli zake na yanatekeleza mateso dhidi ya wananchi raia wa Jamhuri ya Afrika ya Kati, eneo la Kaskazini mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), na Kusini mwa Sudan.
- Katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wanamgambo wenye kujitegemea wa ndani ya taifa hilo, wapiganaji wa kundi la Majeshi ya Demokrasia kwa ajili ya

Wanaendelea kuwa majeshi yenyewe kuyumbisha katika eneo la mashariki mwa nchi.

Changamoto Kimataifa

Vitisho kwa ushwari havijionyesi vyenye katiya migogoro, lakini vinaweza kuwa na ushawishi mbaya kwa maendeleo ya utawala bora, uchumi wa masoko huru, na athari kwa sekta za ulinzi. Mataifa yenyewe kutawaliwa kwa udhaifu yanaleta mazingira yenyewe kutakiwa kivitendo na watumiaji nguvu wenyewe siasa kali, uharamia, usafirishaji haramu wa binadamu, silaha, na dawa za kulevyo, na kusababisha vitisho ndani ya taifa la Marekani na kwa maslahi yetu nchi za nje.

Siasa kali za Utumiaji Nguvu

Siasa kali za utumiaji nguvu zenyewe kufanywa na makundi ya kigaidi ya kimataifa ni chanzo cha kutokuwepo ushwari katika mataifa. Katika mwaka uliopita, al-Qaeda na makundi mengine ya kigaidi katika Afrika yanaonekana yaliimarishta ushirikiano wake. Wafuasi wa al-Qaeda wanashughulika katika Afrika ya Mashariki, wakati al-Qaeda katika mataifa ya Kiislamu ya Kiarabu, (AQIM) inaendelea kushughulika katika eneo la kaskazini na magharibi mwa jangwa la Sahara. Viongozi wa kundi la Al-Shabaab nchini Somalia wamejiunga wazi wazi na kundi la al-Qaeda, na walitowa taarifa hadharani kumsifu Osama Bin Ladin na kuihusisha Somalia na shughuli za dunia mzima zenyewe kufanywa na al-Qaeda. Al-Shabaab vile vile ilitangaza uungaji wake mkono kwa al-Qaeda katika eneo la Peninsula ya Arabia (AQAP) wakati huo huo shughuli za AQAP zimeongezeka nchini Yemen, ambayo imetengwa na Somalia kwa umbali wa maili 20 za upana na mlango wa bahari wa Bab-el-Mandab. Al-Shabaab inaendelea kuendesha kambi nyngi za kufundishia magaidi nchini Somalia huku al-Qaeda ikishiriki.

Al-Qaeda na washirika wa al-Qaeda vile vile wanailenga Marekani na washirika wetu wa Ulaya na washirika wetu wa Afrika katika Kaskazini mwa Afrika na eneo la Sahel. Shughuli za kigaidi, utekaji nyara wa watu, usafirishaji haramu wa aina zote (binadamu, silaha, dawa za kulevyo), na kuwepo kwa mataifa yenyewe kutawaliwa kwa udhaifu katika eneo la Sahel vyote vinachangia hali ya uwezekano wa kudhuriwa na inasababisha uwezekano wa kufanyika ushawishi wa siasa kali.

Nchi za Kiarabu Afrika kama vile Algeria na Marocco zinaungana na Marekani katika kupambana na ugaidi na kukaguwa upanuzi wa magharibi wa kundi la al-Qaeda na washirika wake. Bila ya shaka, upanuaji wa shuguli za ulinzi hutegemea ushirikiano wa mataifa na upanuaji wa maendeleo ya uchumi kwa ushwari ili kukabiliana na kuzuia shughuli za uandikishaji wa watu kuwaingiza katika vyama na makundi yenyewe siasa kali yenyewe kutumia nguvu.

Usafirishaji Haramu

Biashara na usafirishaji haramu wa dawa za kulevyta ni swala lenye kuendelea kuleta wasi wasi katika Afrika. Afrika ya Magharibi ni kifundo cha dawa za kulevyta zinazotoka nchi za Latin Amerika kwenda katika masoko katika nchi za Ulaya. Zaidi ya hivyo, dawa za kulevyta katika nchi za Asia zinasafirishwa kupitia Kusini na Mashariki mwa Afrika zikiwa njiani kwenda Ulaya. Ushawishi wenyewe kuyumbisha na kuharibu wenyewe kutokana na biashara ya usafirishaji haramu wa dawa za kulevyta unatishia kuigeuza Guinea-Bissau kuwa nchi ya dawa za kulevyta na kusaidia kupanua vituo na ushawishi wa matajiri wauzaji haramu wa dawa za kulevyta wa nchi za Latin Amerika kote Afrika. Nchi nyingi za Afrika hazina uwezo wa kukabiliana na uingizaji nchini wa dawa za kulevyta kupitia njia za ardhini, angani au baharini. Wakati haziwaathiriwa moja kwa moja na uingiaji wa dawa za kulevyta kote Afrika kama vile zilivyoathirika nchi washirika wetu katika Ulaya, Marekani ina maslahi yake katika kukabiliana na athari zenye kuyumbisha za biashara na usafirishaji haramu wa dawa za kulevyta dhidi ya ulinzi, ushwari, na maendeleo katika Afrika.

Waafrika wengi bado wanabakia katika hali ya uwezekano wa kudhurika kutokana na biashara haramu ya kusafirisha binadamu kwenda kufanya kazi za kitumwa, kuwafanyisha kazi watoto wadogo, wanajeshi watoto, na utumwa. Wakati baadhi ya nchi zinafikia mafanikio katika mapambo dhidi ya biashara ya usafirishaji wa watu, nchi nyingi zinakosa uwezo wa jeshi la kupambana na tatizo hili.

Uharamia

Vitendo vya uharamia katika Pembe ya Afrika na Ghuba ya Aden vimeendelea kushughulikiwa na jamii ya kimataifa. Mwaka 2009, mashambulio ya maharamia yaliendelea kuenea na kutokea mara nyingi na kupanuka katika eneo la kijografia katika magharibi ya bahari ya Hindi nje kiasi cha maili 1,000 za baharini kutoka pwani ya Afrika. Kikosi cha Jeshi Maalumu la Marekani Afrika kinaendelea kuunga mkono operesheni za kupambana na uharamia kwa kutumia vyombo vya angani visivyokuwa na marubani pamoja na ndege za doria za jeshi la majini ambazo zimeweka kambi ya muda katika nchi ya Ushelisheli.

Afyaya Umma, Maendeleo ya Kiuchumi, na Uletaji Demokrasia

Afyaya Umma, Maendeleo ya Kiuchumi, na Uletaji Demokrasia ni changamoto ambazo zinaendelea kuleta athari kubwa kwa hali ya mazingira ya ulinzi katika Afrika.

Sekta ya Afya ya Umma

Wakazi wa nchi za Afrika wanaendelea kukabiliwa na uwezekano mkubwa wa kuathiriwa na magonjwa mengi ya kuambukiza, pamoja nayo, ugonjwa wa mafua ya nguruwe, H1N1uliotokea mwaka 2009. Virusi vya ugonjwa wa ukimwi na ugonjwa kamili wa ukimwi

(HIV/AIDS), kifua kikuu, na malaria ni chanzo kikuu cha vifo vya watu wa umri mkubwa katika Afrika. Nchi nyingi za Afrika hazina uwezo wa kutosha wa kuzuia au kupunguza kitisho cha magonjwa ya halaiki.

Magonjwa ya halaiki, siyo swala la ulinzi wa binadamu peke yake, bali pia ni changamoto kwa uwezo wa majeshi kuwa tayari. Kwa mfano, baadhi ya washirika wetu wa Afrika wana majeshi ya kitaalamu na uwezo ambao wanachangia maelefu ya wanajeshi wake kwa misheni za Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika nchini Somalia, Sudan, DRC, na kwengineko. Hata hivyo, nchi hizo zingekuwa na majeshi yenye uwezo zaidi wa kulinda amani kama kusingekuwepo kiwango kikubwa cha maambukizo ya virusi vya ukimwi na ugonjwa kamili wa ukimwi (HIV/AIDS) ambacho kinaathiri wanajeshi wao wengi.

Maendeleo ya Kiuchumi

Hadi kutokea kwa matatizo makubwa ya kiuchumi ya dunia mzima mwishoni mwa mwaka 2008, Afrika kwa jumla ilikabiliwa na miaka kumi ya maendeleo ya kiuchumi yenye kuendelezwa, ikiwa ni ya kiwango zaidi ya asilimia 5 kila mwaka. Bei ya juu ya mafuta iliziruhusu baadhi ya nchi za Afrika zenye kuzalisha mafuta kupata maendeleo ya kiuchumi ambayo yalishindana na viwango vya juu kabisa duniani. Hata hivyo lakini, nchi ambazo zinategemea mafuta peke yake na mapato ya bidhaa za uziduaji peke yake zilikabiliwa na hali ya kushuka kwa bei. Katika kesi nyingi, unakuta kwamba uchumi ambao haukupanuliwa, idadi kubwa ya watu wasio na kazi, na ulaji rushwa uliokithiri, yote yamezuia utajiri ambao umetolewa na mali asili za Afrika kuwafikia idadi kubwa ya watu wenye kuhitaji zaidi katika jamii za Kiafrika. Umoja wa Mataifa uliitambuwa Afrika kuwa ni bara fukara zaidi, likiwa na nchi 25 fukara sana duniani.

Uletaji Demokrasia

Katika muda wa miaka 20 iliyopita, nchi nyingi za Afrika zimeanzisha mfumo wa demokrasia, utawala bora, na utiifu wa sheria. Januari mwaka 2009, wananchi wa Ghana waliendesha uchaguzi wao wa rais wa nne huru na wa haki katika muda wa miaka 15. Kwa mara ya pili, chama tawala kilinyang'anywa madaraka kwa amani na upande wa upinzani. Aprili mwaka 2009, zaidi ya wananchi 13 milioni wa Afrika ya Kusini walipiga kura na wakamchaguwa Jacob Zuma, kuwa rais wa nne tangu kumalizika kwa mfumo wa ubaguzi wa rangi nchini humo, na Botswana, Octoba mwaka 2009 ilifanya uchaguzi wake wa kumi wa kidemokrasia kumchaguwa rais tangu nchi hiyo ijipatie uhuru wake – uchaguzi ambao umefanyika mara nyingi zaidi ya nchi yoyote ile ya Afrika kusini mwa jangwa la Sahara. Tangu miaka ya 1990, nchi nyingi za Afrika vile vile zimeondoka kutoka mfumo wa kimabavu na kidikiteta na kuanzisha mfumo wa demokrasia.

Sekta ya Ulinzi Afrika

Ingawaje nchi za Kiafrika zimeelezea mara nyingi nia kubwa ya kudumisha ulinzi wake na kukabiliana na kukabiliana na changamoto hizi mbali mbali wao wenyewe, nchi nyingi zinakosa uwezo wa kufanya hivyo bila ya msaada kutoka nchi za nje. Changamoto zenye kuzikabili nchi za Afrika zinaweza kuelezwaka kama hivi:

- Majeshi mara nyingi yametumiwa kama vyombo vya serikali za kimabavu za kidikiteta ili kulinda viongozi wake na kuzimisha wapinzani. Na hii imesababisha ulaji rushwa na wananchi kupoteza imani zao.
- Hatua za kuleta utaalamu kwa majeshi mengi ya Afrika zinaendelea kuwa kazi yenye kuendelezwa. Kwa asili, maendeleo ya majeshi ya majini na angani ya nyuma kulinganisha na maendeleo ya majeshi ya ardhini katika majeshi mengi ya Afrika.
- Hiba ya siasa za Vita Baridi ziliivamia Afrika zikipata silaha na vifaa vyenye kushindana, harakati za kijeshi na mafundisho ya kijeshi. Mengi ambayo yamebakia yanafanya kazi kwa udhaifu na hayafai kitu katika kukabiliana na changamoto za miaka hii ya leo.
- Ingawaje ushirikiano wa nchi na nchi katika Afrika umeimarika kwa kiasi kikubwa, juhudzi za pamoja za kukabiliana na changamoto za kimataifa ni duni. Siasa za ndani ya nchi zinaweza kuzuia nia ya serikali ya kutaka kuchukuwa hatua kali dhidi ya vyama na makundi yenye siasa kali yenye kutumia nguvu au vitisho vingine vya moja kwa moja.
- Jeshi lenye Kujiweka Tayari la Afrika lililopo chini ya Umoja wa Afrika pamoja na brigedi zake tano limeonyesha maendeleo yenye kuendelezwa, lakini bado hayajawa na uwezo kamili wa kushughulika katika misheni. Majeshi hayo yanakosa uvezeshaji wa kutosha ili kuweza kujitegemea wenyewe kama jeshi la kulinda amani na jeshi lenye uwezo wa kukabiliana na maafa. Uwezo wa kulinda amani ndani ya nchi vile vile unakosekana, ingawaje baadhi ya nchi zimechangia mara kwa mara na mchango mkubwa wa wanajeshi kwa misheni za kulinda amani za kimataifa.

MTAZAMO WA KIKOSI CHA JESHI LA MAREKANI AFRIKA

Mtazamo wetu unatokana na maslahi yetu ya ulinzi wa taifa katika bara hilo la Afrika kama vile ilivyolezwa na Rais na Mawaziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ulinzi. Marekani na

washirika wetu wa Afrika wana maslahi makubwa ya pamoja katika kuleta ulinzi na ushwari katika bala la Afrika na nchi za visiwa, na maeneo ya bahari. Katika kuleta maslahi hayo inatakiwa mtazamo wa pamoja ambao unaunganisha juhud zetu na zile za wizara nyingine za serikali ya Marekani, idara za serikali, na washirika wetu wa Afrika na washirika wengine wa kimataifa.

Mipango yetu na shughuli zetu zinaunga mkono maslahi ya taifa la Marekani pamoja na kufuatilia malengo manne yenyе kuhusika na ulinzi ambayo yametolewa na washirika wetu wa Afrika:

Kwanza, kwamba wao wawe na majeshi yenye uwezo na yenye kuwajibika ambayo yatakeleza kazi zake kiutalaamu na uadilifu;

Pili, kwamba majeshi yao yawe yanaungwa mkono na kuendelezwa na taasisi zenye ufanisi, halali, na ulinzi wa kitaalammu;

Tatu, kwamba wawe na uwezo wa kutekeleza hatua za kitaifa na kwa ushirika na nchi nyingine jirani katika kugeuza mawazo na nia, kuzuia na kuvishinda vitisho vya kimataifa;

Nne, kwamba ziwe na uwezo wa kuongeza uungaji mkono wao kwa juhud za kulinda amani kimataifa.

Kuleta ushwari huunga mkono juhud za kutekeleza malengo haya, na kunatowa fursa zaidi ya kuleta mafanikio.

Mtazamo wetu upo chini ya malengo ya sera za jumla za serikali ya Marekani. Sisi tunafanya kazi kwa ushirikiano na washirika wetu wa ndani wa idara mbali mbali, kama vile Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani (DOS) na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Marekani (USAID), ili kuhakikisha mipango yetu na shughuli zetu zinaunga mkono moja kwa moja malengo ya sera za nchi za nje za Marekani.

Changamoto za Afrika zinahitaji mkabala wa jumla kuhusu usalama ambao ni pamoja na ulinzi, utekelezaji wa sheria, na usalama wa forodha na mipakani. Katika kukabiliana na changamoto za maswala ya ulinzi ni lazima zifuatiliwe kwa ushirikiano na juhud nyingine za serikali na Marekani na shughuli za usalama za washirika ili kudumisha juhud za umoja.

Shughuli zetu ni lazima zitowe manufaa ya mara moja na kusaidia washirika wetu kuendeleza malengo yao ya muda mrefu. Misheni yetu sisi ni “shughuli za usalama zenye kuendelezwa;” Kutowa mipango na shughuli ambazo zinajenga hali ya baadaye na kuleta mafanikio.

Mafanikio ya nchi na nchi ni muhimu sana, ziwe ni nchi jirani zikifanya kazi pamoja dhidi ya vitisho vya pamoja, au juhud za nchi mbali mbali za kuanzisha ushirika wa pamoja katika maswala ya ulinzi, kama vile ushirikiano wa ulinzi wa Umoja wa Afrika. Mtazamo wetu

unazingatia maslahi ya wote, kuleta uwezo wa utekelezaji na utambuzi wa hali ya kawaida, ujenzi wa uwezo wa nchi na nchi, na kuhimiza ushirikiano wenyewe kujengwa chini ya msingi wa kuaminiana na kushirikiana. Kadri nchi za Afrika zinavyofanya kazi kwa pamoja ndivyo uwezekano unavyokuwa mkubwa wa kuleta ushwari wa kudumu katika bara hilo.

Malengo haya yanaunga mkono maslahi ya ulinzi wetu wa taifa. Kuongeza uwezo wa washirika wetu Afrika katika kutambuwa na kuingilia kati vitisho vinavyotoka katika bara hilo kunazidisha usalama wa taifa la Marekani. Kuhimiza uwezo wa majeshi ya Afrika katika kukabiliana na vitisho dhidi ya amani na ushwari katika bara hilo kunaipa fursa Marekani kutumia majeshi yake katika operesheni nyingine. Ujenzi wa majeshi yenyewe uwezo wa kitaalamu unaweza kuunga mkono juhudhi za kudumisha misingi ya kidemokrasia na utawala bora kwa kuhimiza uwazi na kuwajibika katika jeshi, ambalo kihistoria limekuwa moja ya taasisi muhimu sana katika jamii ya kisasa ya Kiafrika.

PROGRAMU NA SHUGHULI ZA KIKOSI MAALUMU CHA JESHI LA MAREKANI **AFRIKA**

Mipango na shughuli za Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika inaunga mkono ujenzi wa majeshi ya washirika yenyewe utaalamu na uwezo, na imechanganywa na huratibiwa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani (DOS), Wakuu wa Misheni wa Marekani, na washirika wetu wa kimataifa. Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika huendesha shughuli kadhaa katika kuunga mkono malengo manne ya msingi na kukabiliana na changamoto za sasa katika swala la usalama ambazo zinatishia ushwari. Madhumuni ya msingi ya shughuli zetu yanaweza kuelezewa kama ifuatavyo:

- Kujenga uwezo wa majeshi ya kawaida ya washirika
- Kuunga mkono ujengaji wa uwezo wa majeshi ya usalama ya washirika
- Kujenga uwezo wa majeshi ya washirika yenyewe kutekeleza
- Kudumisha na kujenga uhusiano mzito wa kimkakati
- Kuleta mageuzi katika seckta ya ulinzi
- Kudumisha uhustiano wa nchi na nchi, utambuzi wa hali, na utekelezaji
- Kupambana na vitisho vya kitaifa na kimataifa vya makundi yenyewe siasa kali
- Kuchangia ushwari katika maeneo yenyewe migogoro hivi sasa
- Kukabiliana na hali ambayo husababisha kutokuwepo ushwari

Ujenzi wa Uwezo wa Majeshi ya Kawaida ya Washirika

Wanajesi wa Marekani wa ardhini, wanamaji, wa angani, na marines ni waalimu wajuzi wenyewe kuonyesha mfano wa utaalamu wa kijeshi na thamini za taifa letu. Mafunzo na mazoezi

ambayo wanaendesha yanahimiza maendeleo ya uwezo wa shughuli za usalama za washirika na kuweka maadili ya kitaalamu mionganini mwa wanajeshi wa Kiafrika. Zaidi ya hivyo, nyingi za shughuli hizi zinaweza kufanya na idadi ndogo ya wanajeshi wa Marekani. Baadhi ya mifano ya shughuli zetu za hivi karibuni ni pamoja na:

ZOEZI MOTO ASILI, Uganda

October mwaka 2009, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika, kwa ushirikiano na Jeshi la Ardhini la Marekani Afrika (USARAF) kama waongozaji, waliwakusanya zaidi ya wanajeshi 1,200 na raia kutoka nchi sita kushiriki katika zoezi lililopewa jina la Moto Asili 10 nchini Uganda. Zoezi hilo liliimarisha uwezo wa utendaji na lisaidia kujenga uwezo wa washirika wetu Waafrika kuwawezesha kujibisha dharura ngumu za kibinadamu. Eneo hilo la Afrika lililweza kwa pamoja kufanya mazoezi ya upangaji wa hatua za kukabiliana na kitisho cha dunia cha ugonjwa wa mafua. Wanajeshi wapatao 550 wa Marekani na wanajeshi 650 kutoka Burundi, Kenya, Rwanda, Tanzania, na Uganda walishiriki katika zoezi hilo.

Kituo cha Ushirika Afrika

Kituo cha Ushirika Afrika (APS) ni shughuli ya msingi ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika katika kudumisha usalama na sasa ni programu yenye sifa. Kwa ushirikiano na nchi washirika pamoja na mashirika yasiyo ya serikali (NGOs), APS hujenga uwezo wa kudumisha usalama mionganini mwa washirika wetu wa Afrika kwa kutumia majukwaa ya mafunzo ambayo hufanyika katika meli zilizopo nje baharini ili kutowa utambulisho wa kuwepo bila ya kuweka nanga ufukoni. Mafunzo yetu na misaada inazingatia haja ya kuimarisha nguzo nne katika maendeleo ya sekta za majini: kutowa jeshi lenye uwezo na utaalamu wa usalama baharini; kuwezesha miundombinu ambayo itaendeleza shughuli za baharini; ufahamu wa shughuli za baharini; na kuwezesha uwezo wa kushughulikia matukio yenye kutokea baharini. Washirika wetu wa Afrika wanakiona kituo hiki cha Ushirika Afrika – APS - kuwa ni hatua yenye mafanikio katika shughuli za baharini na ni washirika wenye kufurahia.

Kuanzia mwezi wa Januari hadi mwezi Mei mwaka 2009, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani kiliitumia manowari USS NASHVILLE kuunga mkono shughuli za APS. Kukiwepo wawakilishi washirika kutoka nchi tisa za Ulaya, nchi 10 za Afrika, na Brazil, APS iliongeza mara mbili washirika wake ambao hushiriki katika kupanga na kutekeleza shughuli kulinganisha na huko nyuma. APS iliendesha mafunzo 10 katika nchi saba – Senegal, Liberia, Ghana, Nigeria, Cameroon, Sao Tome na Principe, na Gabon. Wanajeshi wa Marines wa Marekani na washirika wake kutoka Uhispania na Ureno waliendesha matukio ya ushirikiano wa ulinzi na usalama na zaidi ya wanajeshi wataalamu 800 kutoka majeshi ya Afrika nchini Senegal, Liberia, Ghana, Nigeria, Cameroon na Gabon. Zaidi ya wanajeshi 1,750 wa Afrika walishiriki katika majopo na semina mbalimbali.

Mafanikio na ufanisi wa shughuli zetu ulionyeshwa wakati jeshi la majini la Benin lilipovamia na kuiachilia huru meli moja ya kubeba mafuta iliyotekwa nyara bila ya kupoteza

maisha ya mtu yoyote yule. APS nchini Benin ilikuwa mtendaji mkuu katika misheni hiyo. Jeshi la majini la Benin lilishiriki katika mafunzo ya APS kuhusu hatua za kutembelea, Ingia ndani, Pekua na Kamata, operesheni dhidi ya boti ndogo ndogo, Mapambano dhidi ya Ugaidi/Ulinzi wa Wanajeshi, na matumizi ya mitambo ya kisasa ya mawasiliano (AIS), ambayo ilisimikwa wakati wa mafunzo yao. Jeshi la majini la Benin lilitumia ujuzi wa utambuzi wa baharini ambao ulitolewa na APS kuiongoza moja ya meli zake katika kuisaidia meli moja ya kubeba mafuta, na hivyo kuliruhusu jeshi lake la Majini kuchukua hatua dhidi ya kitisho chenye kuliathiri taifa la Benin, Marekani, na jamii ya kimataifa.

Jeshi la majini la Marekani, Africa (NAVAF), linajenga nguvu zake kutokana na mafanikio ya APS katika Afrika ya Magharibi kwa kuendesha shughuli kama hizo katika Afrika Mashariki. APS-Mashariki itafanya kazi ya kujenga uwezo kwa washirika wetu katika operesheni za boti ndogo ndogo. Washirika wetu ni pamoa na Kenya, Msumbiji, Ushelisheli, Mauritius na Tanzania. Shughuli za manowari za Marekani USS BRADLEY na USS ARLEIGH BURKE katika mwaka 2009 zilifanya kazi kama meli waanzilishi kwa shughuli za APS-Mashariki na zilifanikiwa sana katika Kusini na Mashariki mwa Afrika. Zaidi ya hivyo, Jeshi la Pamoa la Shughuli Maalumu la Marekani katika Pembe ya Afrika (CJTF-HOA) lilianzisha kutuo cha baharini katika mji wa Mombasa nchini Kenya, ili kutowa mafunzo kwa nchi za Afrika. Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Wizara ya Ulinzi ya Marekani, zote zilipitisha sehemu ya sheria fungu 1206 (Mwaka wa fedha 06 sheria ya Mamlaka ya Ulinzi wa Taifa, kama ilivyorekebishwa) mpango ambaو ulilengwa kutowa boto ndogo, AIS, na rada za upekuzi ardhini kwa Djibouti, Msumbiji, Kenya, Tanzania, Ushelisheli, Mauritius, na Comoro. Juhudi hii ya mwisho itasaidia kuleta uwezo wa msingi wa doria katika eneo zima la pwani ya Afrika ya Mashariki. Tunapanga kudumisha na kuimarisha zaidi mradi huu kupitia kitengo cha Utowaji Fedha kwa Majeshi ya Nchi za Nje cha Jeshi la Marekani (FMF).

ZOEZI LA SIMBA WA AFRIKA, Morocco

Simba wa Afrika ni zoezi la kila mwaka linalofanywa kati ya Marekani na Morocco ambayo ni mshirika muhimu na mchangiaji mkubwa katika operesheni za kulinda amani za kimataifa. Majeshi ya Majini ya Marekani, Afrika (MARFORAF) ni kitengo kikuu cha Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika katika zoezi hilo ambalo linazingatia utendaji wa majeshi ya Marekani na Morocco, mafunzo ya kijeshi ya angani na ardhini ya silaha, mafunzo ya maafisa, mafunzo kuhusu operesheni za kulinda amani (PKO), mafunzo ya utowaji huduma za tiba na maafa, mafunzo ya maswala ya umma, na operesheni za misaada ya kibinadamu kwa raia. Mwaka jana, wakati wa zoezi la Simba wa Afrika 09, timu ya wanajeshi wa tiba waliendesha shughuli za misaada ya kibinadamu kwa raia katika viji vitano, na kuwatibu Wamorocco zaidi ya 17,000 na zaidi ya mifugo 9,500. Mazoezi mbali mbali katika mwaka wa fedha wa 2010-2011 yenye kuhusu miradi ya ujenzi yamepangwa kufanyika ili kuimarisha mapana ya mazoezi, mafanikio ya kimkakati, na utowaji wa huduma za utaratibu wa ugavi na usafirishaji ili kuunga mkono shughuli za zoezi hilo la Simba wa Afrika. Jeshi la Angani la Marekani Afrika (AFAFRICA) litahimiza kushiriki kwake katika zoezi hilo la Simba wa Afrika

kupitia Mpango wa Ushirika wa Taifa, wakati Jeshi la Ulinzi wa Taifa la Marekani la jimbo la Utah likitowa wanajeshi wake na vifaru vya kivita aina ya KC-135.

Ujenzi wa Maafisa wenye Ufanisi Wasiokuwa Maafisa wa Juu Waliofuzu (NCO)

Nchi kadhaa za Afrika zina wanajeshi wasiofuzu kuwa maafisa wa jeshi, na kwa hali fulani fulani wanashawishika na rushwa. Washirika wetu wa Afrika wanatambuwa kwamba maafisa wasiofikia mafunzo na vyeo vya uofisa jeshini ni muhimu sana katika ujenzi wa vikosi vya jeshi vyenye kuijendeleza, ambavyo vitachangia katika swala zima la usalama na ushwari. Nchi hizo za Afrika zimetuomba msaada wetu. Kwa kuwasaidia washirika wetu kujenga vikosi vya wanajeshi ambao hawakufikia vyeo vya juu (NCO), sisi tunakuwa na fursa ya kujenga hadhi na maadili ambayo yatawaruhusu washirika wetu kutowa mafunzo na mwongozo wa maendeleo yao katika upande huu.

Utowaji wa Fedha kwa Majeshi ya Nje (FMF) na Mauzo ya Kijeshi Nchi za Nje (FMS)

Changamoto kubwa ambalo linawakabili washirika wetu wengi ni ukosefu wa silaha na vifaa vya kijeshi vyenye kufanya kazi kwa ufanisi – kuanzia vifaa vya kijeshi vya mwanajeshi binafsi hadi magari ya kijeshi na mashine na mitambo mingine mikubwa. FMF na FMS ni mipango miwili ambayo tunaitumia kusaidia kukabiliana na upungufu huu. Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinafanya kazi na timu za Marekani katika kutunga na kutekeleza mipango ya utowaji wa fedha kwa majeshi ya nchi za nje (FMF) ili kutowa mitambo ambayo itaongeza uwezo wa kijeshi mionganoni mwa washirika wetu wa Afrika, washirika wetu wa kimataifa, na Marekani pia. Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinatumia mpango kabambe chini ya Mauzo ya Kijeshi Nchi za Nje (FMS) ili kutowa malori, vifaa binafsi vya wanajeshi, sare za kijeshi ili kuunga mkono batalioni za wanajeshi wa kulinda amani wanaopelekwa Darfur nchini Sudan, Somali, na Liberia.

Kuunga Mkono Ujenzi wa Uwezo kwa Majeshi ya Washirika ya Kulinda Usalama

Swala la kuwa na ushwari na usalama katika Afrika linahitaji zaidi ya michango kwa majeshi peke yake. Usalama ni mkabala wa jumla ambao unajumuisha mambo yasiyo ya kijeshi kama vile utiifu na utekelezaji wa sheria, doria mipakani, ushuru wa forodha na mahakama. Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinafanya kazi kwa karibu sana na Wizara za Serikali ya Marekani na Idara zake ili kuhakikisha kwamba tunapanga na kuendesha juhudzi zetu bila ya matatizo inavyowezekana.

Ushirikiano na Afrika katika Utekelezaji wa Sheria za Baharini (AMLEP)

AMLEP ni mpango wa ushirikiano wa utekelezaji wa sheria za baharini kati ya Afrika na Wizara ya Usalama wa Taifa ya Marekani. Jeshi la Ulinzi wa Pwani ya Marekani na nchi mwenyeji wa Kikosi cha Utekelezaji wa Sheria (LEDET) hukabiliana na meli za Marekani na za nchi wenyeji na boti au meli za kikosi cha Utekelezaji wa sheria za nchi ili kutowa mamlaka yenye kuhitajika kwa meli na uwezo wa kuingia na kupekuwa, kukamata, na kuwatia nguvuni

watu katika eneo la nchi za Afrika ambazo zinajulikana kuwa maeneo maalumu ya kiuchumi (EEZ).

AMLEP shughuli zake zilifanyika nchini Senegal, Morocco, Sierra Leone, na Cape Verde, kwa msaada wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani, Majeshi ya Angani yenye kushughulika baharini, na Jeshi la Ulinzi wa Pwani wa Marekani. Kwa pamoja, operesheni zetu zilifanikisha yafuatayo: Utekelezaji wa sheria za baharini na mafunzo ya boti ndogo kwa maafisa wa LEDET; kuunganishwa kwa shughuli na uwezo wa ndege za Jeshi la Ufaranza zinazoshughulika maeneo ya baharini; na hatua ya kuingia ndani ya meli au boti hatua zenyenye kuongozwa na timu ya nchi husika ya LEDET.

Kilele cha hatua zetu kilitokea mwezi Augosti wakati Jeshi la Majini la Jamhuri ya Sierra Leone lilipoitia nguvuni meli ya tani 750 ya Taiwan iitwayo F/V YU FENG 102 kwa makosa ya kuvua samaki kinyume cha sheria nchini Sierra Leone eneo maalumu la kiuchumi (EEZ). Mabaharia 11 wa meli hiyo YU FENG walifukuzwa na kurudishwa nchini Taiwan na meli ilizuiliwa na serikali ya Sierra Leone. Majeshi ya Sierra Leone yalionyesha ushujaa wake tena na uwezo wake kwa kuziteka meli nne kwa makosa ya kukiuka sheria za Sierra Leone wakati wa mazoezi ya AMLEP yaliyofanyika mwezi Desemba.

Makadirio ya Sekta ya Usalama

Makadirio yenye kuchanganywa kuhusu matakwa ya taifa shirika husaidia katika kutunga shughuli zenyenye ufanisi na zenyenye kushirikishwa. Katika mwaka huu uliopita, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kilishiriki katika Makadirio ya Sekta ya Ulinzi yaliyoendeshwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani nchini Senegal, Guinea-Bissau, Ghana, Togo, Sierra Leone, Liberia, Cape Verde na Msumbiji. Matokeo ya ushirikiano huo wa mipango ya Wizara na Idara yatahakikisha kwamba shughuli zetu za kijeshi na nchi hizo za Afrika zinakwenda sambamba na malengo ya sera na kwa pamoja, zitaunga mkono shughuli za wizara na idara nytingine za serikali ya Marekani.

Ujenzi wa Uwezo wa Majeshi ya Utendaji ya Washirika

Watendaji kama vile wanajeshi wanaoshughulikia utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa wato na vitu, upelelezi na ujasusi, mawasiliano, na uwezo wa kutengua mabomu, ni watu wenye majukumu muhimu sana katika jeshi la Marekani, nao wanatoa huduma na uwezo wetu wa kuendeleza operesheni kwa uhuru. Katika kuwajenga watendaji sawa na hao au kuwezesha uwezo huo mionganoni mwa nchi za Kiafrika kunaweza kusaidia kupunguza tegemezi lao kwa misaada ya nchi za nje wakati wanapoendesha operesheni za kijeshi. Nyingi ya ujenzi wetu wa uwezo na utendaji katika pande hii unaongeza thamani kubwa sana wakati ni wanajeshi wachache wa Marekani wanatumwiwa.

Ujenzi wa uwezo wa huduma ya utaratibu wa ugavi na usafirishaji

Washirika wetu wa Afrika wanatambuwa umuhimu wa ugavi na usafirishaji na wamenufaika kutoka matukio ya mafunzo kadhaa yaliyotolewa na Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika pamoja na semina mbali mbali kwa upande huu. Kwa mfano, watalaamu kutoka kundi la U.S. MARFORAF walitowa msaada muhimu wa ugavi na usafirishaji kulisaidia jeshi la ardhini la Sierra Leone kufungasha na kupakia vifaa vyao katika meli moja ya Umoja wa Mataifa katika matayarisho yao ya safari yao ya kwanza ya misheni ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kulinda amani katika eneo la Darfur, Sudan (UNAMID).

Timu ya Ushirika wa Msaada wa Upelekaji Wanajeshi Afrika (ADAPT) huunda uwezo na utaratibu wa ugavi na usafirishaji kwa majeshi ya Afrika ili kuyawezesha kukabiliana na juhudzi zake za operesheni za kulinda amani. Mafunzo ya ADAPT yenye kutolewa na Jeshi la Ardhini na Angani lililopo chini ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika yaliliwezesha Jeshi la Ulinzi la Rwanda kupakia na kufikisha magari yake ya kijeshi na vifaa na chakula hadi Sudan kusaidia juhudzi za kulinda amani (UNAMID) katika Darfur. ADAPT vile vile iliwezesha Jeshi la Ulinzi la Wananchi la Uganda kuwawezesha wanajeshi wa Uganda kupakia vifaa vyao vya kijeshi katika ndege za kijeshi za Marekani (C-130 na C-17), na hivyo kuimarisha uwezo wao wa kusaidia na kuunga mkono juhudzi za kulinda amani na operesheni za kusaidia katika maafa kwa kutumia ndege za kijeshi za kubeba mizigo za Marekani au ndege za kubeba mizigo za Umoja wa Mataifa. Wanajeshi hawa pia watakuwa waalimu washirika katika shughuli za ADAPT. Shughuli za ADAPT zimepangwa kufanyika nchini Nigeria na Tanzania katika mwaka huu wa 2010.

Katika mwaka 2009, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kiliendesha semina yake ya kwanza ambayo ulihusu *Ushirikiano kwa ajili ya Kusaidia shughuli za Ugavi na Usafirishaji, Operesheni na Mikakati yake (PILOT)* kwa washirika 25 wa nchi za Afrika. PILOT ni semina ya kiwango cha operesheni ambayo imebuniwa kwa pamoja na kugharimiwa na Wizara ya Ulinzi ya Canada, na Kituo cha Kulinda Amani cha Pearson nchini Canada. PILOT huzingatia maswala ya sheria na maadili katika shughuli za kulinda amani; majukumu, misheni, na kazi za kulinda amani za Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa; kupanga makadirio ya ugavi na usafirishaji kwa niaba ya PKO; Kupanga Makaribisho, Utayarishaji, Usafirishaji, na mchanganyo wa operesheni; ubunifu wa utawanyaji wa wanajeshi na utekelezaji wake; na mpango mzima wa shughuli za operesheni za pamoja.

Ujenzi katika Upande wa Upetelezi

Upetelezi wa kijeshi ni muhimu sana kwa uwezo wa majeshi ya kitaalamu ya kisasa. Uwezo wa kukusanya, kutathimini na kusanisi habari ni mambo muhimu katika kujenga mipango ya kijeshi yenye ufanisi.

Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika katika mpango wake wa *Ushirikiano wa Upelelezi na Usalama na Utendaji* (ISCE) kinajitahidi kujenga uwezo wa upelelezi wa kijeshi katika mataifa washirika na kati ya nchi na nchi. ISCE inaendesha na kutekeleza mafunzo ya kawaida ya upelelezi wa kijeshi na utekelezaji wake. Inasisitiza umuhimu wa sheria, heshima kwa haki za binadamu, na utawala wa kiraia ili kugeuza shutuma ya kihistoria ambayo ilihuisha shughuli nyingi za upelelezi za nchi za Afrika. Shughuli za mpango ni pamoja na semina za ufahamisho; ziara za maafisa wa ngazi ya juu wa upelelezi; mikutano ya Wakurugenzi wa Upelelezi wa Kijeshi; mabadilishano ya upelelezi na tathimini yake; na mafunzo mbali mbali ya upelelezi kwa maafisa wa jeshi ambao hawakufuzu ngazi ya juu.

Mafunzo ya Kimsingi ya Upelelezi wa Kijeshi kwa Maafisa – Afrika (MIBOC-A) ni mafunzo ambayo yanatolewa kwa maafisa wa ngazi ya chini wa upelelezi wa jeshi, kaskazini na magharibi mwa Afrika. Mbali na kufundisha ujuzi wa upelelezi wa kitaalamu, mafunzo hayo yanahimiza uhusiano baina ya jamii ya upelelezi na kuhimiza pia ushirikiano wa siku za mbele. Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kiliendesha mafunzo mara mbili ya MIBOC-A katika mwaka wa fedha wa 2009 na moja katika mwaka huu wa fedha wa 2010.

Uendelezaji Wa Mifumo Ya Mawasiliano

Njia moja ya kudumisha ushirikiano kati ya nchi na nchi katika Afrika ni kuunda mbinu ambazo wanajeshi washirika wanaweza kuwasiliana kwa kuaminika na kwa ufanisi baina yao. Hata hivyo, kwa sababu miundombinu ya mawasiliano katika Afrika haijainuka, Kikosi Maalummu cha Jeshi la Marekani Afrika kinaunda mipango ambayo itaweza kuimarisha mawasiliano mionganoni mwa viongozi wa kijeshi wa Afrika.

Mfumo wa Mamlaka, Udhibiti, Mawasiliano na Habari wa Umoja wa Afrika ni juhudi ya kuwezesha mamlaka ya Umoja wa Afrika kudhibiti jeshi lake la tahadhari. Mfumo huu ulipata mafanikio yake ya kwanza katika ufunguzi rasmi wa kituo chake kipycha Operesheni za Amani za Umoja wa Afrika, na utaendelea kuunda mamlaka kama hayo na udhiti wake katika makao makuu ya majeshi ya tahadhari, mipango na ugavi. Mfumo huu pia unaendesha juhudi ya kujishughullisha na misheni ya Umoja wa Afrika nchini Somalia (AMISOM).

Tunaendesha pia mipango mingine miwili katika eneo la Afrika. Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) katika upande wa Mabadilishano ya Habari baina ya nchi wanachama katika Nyanja za internet, na huduma za simu kwa viongozi wa ngazi za juu wa kijeshi katika nchi 11 wanachama wa ECOWAS, na nchi hizo zitaongezeka na kufikia 13 hivi karibuni. Wakati huo huo, Juhudi za Kimataifa za Kushirikisha Habari ndio kwanza zimeanza, na zitatowa uwezo wa mawasiliano ya hapa na pale katika Operesheni ya Kudumisha Uhuru-kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara (OEF-TS) katika miaka mitatu ijayo.

Ujengaji Wa Uwezo Wa Kutengua Mabomu

Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinaendesha mafunzo ya “Kumfundisha Mfundishaji” misheni za *Hatua za Kibinadamu dhidi ya Mabomu ya Kutegwa Ardhini* ili kujenga uwezo wa washirika wetu katika shughuli za kutengua mabomu pamoja na kuunga mkono hatua za Marekani na za kimataifa za kuondowa mabomu ya kutegwa ardhini na mabomu mengine yenyе kubakia baada ya vita. Tuliendesha mipango hiyo nchini Kenya, Burundi, Msumbiji na Namibia mwaka 2009, na tutapanuwa mipango hiyo ya kutengua mabomu kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Senegal na Chad katika mwaka 2010. Vile vile, tunashughulika nchini Uganda kujenga uwezo wa kutengua mabomu kuunga mkono juhudи za Uganda za kuendeleza amani AMISOM.

Mipango Maalumu kwa Wanajeshi

Juhudi za kuunda jeshi lenye uwezo zinahusu njama ambazo zinaruhusu uongozi wa jeshi wa nchi wanachama kuunda na kutekeleza mifumo ya uendeshaji na matayarisho ya tahadhari. Mifumo hii inabidi iwe ya uwazi ili kuhakikisha huduma za usawa, haki na mategemeo ya kawaida. Kupitia tegemezi la waongozi na mabadilishano ya habari, mkaguzi wetu mkuu, wachungaji wa kijeshi wa dini, wanasheria, madakitari, na maafisa wa shughuli za umma, na maafisa wengine maalumu wanafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu sana na nchi washirika ili kujenga uwezo katika nyanja hizo ili kuunga mkono uimarishaji wa msimamo wa jeshi na serikali na wananchi wake.

Udumishaji wa Uhusiano Mkubwa wa Kimkakati

Uhusiano wa kimkakati wenye nguvu ni utendaji muhimu wa kudumisha mafanikio muhimu ya uwezo wa shughuli za ujenzi. Unajenga na kuwashimiza washirika wetu kuanza kutumia uwezo wao mpya walioupata na kuutekeleza. Unawahimiza washirika wetu kutumia uwezo wao mpya walioupata. Unatowa fursa ya kuhimiza mafanikio kupitia mwandamo wa mawasiliano wazi ambayo yanatowa na kushughulikia mahitaji mapya au yenyе kuendelea. Yanaruhusu pia mjadala baina ya washirika.

Mpango wa Jeshi la Ulinzi wa Ndani ya Nchi la Marekani na Washirika

Mpango wa Jeshi la Ulinzi la Ndani la Marekani ni chombo kabambe cha kudumisha uelewano wa jeshi kwa jeshi, jeshi kwa raia, na raia kwa raia kwa kutumia uwezo wa Jeshi la Ulinzi wa Ndani wa Marekani na uwezo wa majimbo ya Marekani. Nchi nane za Kiafrika zinashirikiana hivi sasa na majimbo ya Marekani kwa kupitia mpango huu: Nchi hizo na

majimbo ya Marekani ni: Tunisia na Wyoming; Morocco na Utah; Ghana na North Dakota; Afrika ya Kusini na New York; Nigeria na California; Senegal na Vermont; Liberia na Michigan; na Botswana na North Carolina.

Manufaa ya mpango huu kwa mwaka uliopita ni mengi na ya kuvutia. Kwa mfano, nchini Tunisia, Jeshi la Ulinzi wa Ndani la Marekani la Jimbo la Wyoming linaisaidia serikali ya Tunisia kushirikisha huduma za rada ya ardhini ya doria kushughulikia operesheni zaidi za doria. Katika Afrika ya Magharibi, Kikosi cha jeshi la Anga la Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika, (AFAFRICA), kilishikiana na Naibu Waziri wa Jeshi la Angani la Marekani mwenye kushughulikia maswala ya kimataifa, Jeshi la Ulinzi la Angani la Jimbo la Tennessee, na Kituo cha ugavi na usafirishaji wa angani cha Warner Robins kushirikisha juhudzi za jeshi kwa jeshi za kujenga huduma za kwanza za ndege za aina ya C-130 nchini Nigeria. Nchini Botswana, Jeshi la Ulinzi wa Ndani la Angani la North Carolina, Marekani lilifanya maonyesho ya mfumo wake wenye uwezo wa kupambana na moto ardhini kutoka angani; swala muhimu sana nchini Botswana kutookana na moto wenye kutokeza kila mwaka nchini hujmo ambayo unaangamiza ardhi ya malisho ya mifugo na maeneno ya makazi ya wanyama pori muhimu sana katika rasilimali ya Botswana.

Mpango wa Ushirika wa majimbo ya Marekani na Afrika na shughuli zake unajenga uwezo mbali mbali kwa washirika wetu Afrika. Uhusiano huo zoefu ambaa unajengwa na mpango huu unaongezea thamini kubwa sana katika juhudzi zetu. Mpango huu ni wa thamani kubwa kwa Kikosi chetu Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika, na sisi tunatazamia kupanuwa mpango huo wakati washirika wetu wa Afrika wanaomba ushirikiano zaidi. Mimi nawaombeni muunge mkono zaidi na zaidi.

Masomo ya Kijeshi ya Kimataifa na Mafunzo (IMET) na Upanuzi wa IMET (E-IMET)

Hatua ya kuyafanya majeshi kuwa ya kitaalamu na kuhimiza thamini za kidemokrasia za mamlaka yenye kuchaguliwa na umma ni mionganoni mwa manufaa ya mipango ya IMET na E-IMET yenye kuongozwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani. Hatua hizi zinajumuisha mipango ya misaada ya kijeshi yenye kutumiwa sana na Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika katika wajibu wake. Kiasi cha wanafunzi 900 wanajeshi na raia kutoka nchi 44 za Afrika walipata elimu na mafunzo nchini Marekani au katika nchi zao ambayo yaligharimu dola za Kimarekani \$19.8 milioni. Wanajeshi maafisa wengi na wanajeshi wa vyeo vya chini waliopitia na kufuzu mafunzo wa IMET wanarudi nchini kwao kujaza nafasi muhimu katika jeshi la serikali za washirika wetu Afrika. Na uhusiano ambaa umejengwa kutookana na mazingira ya kisomi moja kwa moja unajenga na kuchangia uhusiano wenye nguvu wa kijeshi baina na nchi na nchi kati ya Marekani na nchi washirika.

Semina ambazo zinagharimiwa na IMET zenye kuendeshwa na Taasisi ya Ulinzi ya Elimu ya Sheria na Kijeshi ya Marekani (MET) kwa ajili ya nchi ya Chad, Cameroon, DRC, Mauritius na Sierra Leone, ziliunga mkono pia uhusiano katika vituo vya Uhusiano wa Kijeshi na Raia MET kwa nchi ya Cameroon, Comoro, DRC, Mauritius na Guinea Bissau. Mipango

endelezi ya IMET na E-IMET ni uwekezaji wetu wa miaka ya mbele, na uungaji mkono wa muda mrefu wa maslahi ya Marekani na uhusiano wake katika bara la Afrika. Ni moja ya mipango tunayoithamini na yenyе kuleta mafanikio makubwa.

Mipango ya Jeshi kwa Jeshi katika utekelezaji

Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinatumia njama ya kuwa na uhusiano wa jeshi na jeshi ili kuimarisha uhusiano muhimu na kuwatambulisha washirika wake juu ya mantiki ya jeshi la Marekani, mikakati yake na maendesho yake ambayo nchi washirika zinaweza kufuatisha katika kukabiliana na changamoto mbali mbali za usalama, pamoja nazo, uendeshaji wa kazi ya kulinda amani na mapambano dhidi ya ugaidi. Mipango ya Jeshi kwa Jeshi vile vile inasaidia washirika katika kuimarisha shughuli za kuyatawanya majeshi, mfumo wa ugavi na usafirishaji, operesheni za kuboresha, ulinzi wa wanajeshi, na uendeshaji wa mipango yao wenyewe. Katika mwaka wa fedha wa 2004, mwaka wa kwanza wa mpango huo, fedha kiasi cha chini ya dola za Marekani 500,000 kilitumiwa Afrika kwa mipango ya Jeshi kwa Jeshi. Hii leo, mpango wa Jeshi kwa Jeshi ni kiungo kikuu cha shughuli za Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika, kikiwa na bajeti ya dola za Marekani \$6.3 na mipango 431 ambayo imepangwa kufanyika katika nchi 40 katika mwaka wa fedha 2010. Huu ni uwekezaji mdogo wenyewe kuleta ufanisi na mafanikio makubwa sana.

Kuendesha Mageuzi katika Sekta ya Ulinzi

Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika ni mchangiaji mkubwa maendeleo ya muda mrefu ya majeshi ya ulinzi ya kitaalamu ikiwa ni sehemu ya sekta kubwa ya usalama y;enyе kuongozwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani.

Liberia

Ili kuzingatia mafanikio yaliyofikiwa chini ya mpango wa Sekta ya Usalama ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kilianzisha mpango wa miaka mitano ya unahisi kwa wanajeshi wa makao makuu ya Jeshi la Liberia (AFL) na brigedi ya 23 ya Liberia. Sasa hivi tuna wanahisi 56 nchini Liberia ambao wanaendeleza ujenzi wa kitaalamu wa jeshi la Liberia – AFL. UHURU WENYE KUENDELEA MBELE ni moja ya juhudzi tatu katika mpango kabambe wa mageuzi katika sekta ya ulinzi nchini Liberia. Tunafanya kazi pia na jeshi la ulinzi pwani ya Marekani ili kusalisaidia jeshi la Liberia kuunda jeshi lenye uwezo kama ule wa jeshi la ulinzi wa pwani ya Marekani, huku afisi ya Waziri wa Ulinzi ya Marekani ikiwa inafanya unahisi kwa Wizara ya Ulinzi ya Liberia.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo

Kutokana na maombi kutoka Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani na kutoka serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinatowa mafunzo na kuipatia vifaa vya kijeshi batalioni moja ya Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (FARDC) katika kuunga mkono malengo ya serikali ya Marekani na kipaumbele ambacho kiliwekwa na bibi Clinton, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Marekani wakati wa ziara yake ya DRC mwezi Augusti mwaka 2009. Sisi tutayasaidia majeshi ya FARDC kutekeleza: 1) uimarishaji wa uwezo wake wa kuongoza, kuendesha, na kudumisha majeshi yake; 2) kuzidisha uwezo wake wa kupeleleza na kuwafikisha mahakamani wanajeshi ambaao wanashutumiwa kukiuka haki za binadamu na uhalifu mwingine; na 3) kupunguza utumiaji nguvu katika mambo ya ngono na utumiaji nguvu mwingine wa jinsia (SGBV) wenye kufanywa na wanajeshi.

Lengo la tatu, usuluhihi katika swala la utumiaji nguvu na uonevu wa jinsia, ni muhimu sana katika kusaidia kuponya vidonda vya migogoro ya nyuma katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Tunafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu sana na timu ya nchi hiyo na Idara ya Maendeleo ya Nchi za Nje ya Marekani (USAID) ili kutambua fursa ambazo zitaruhusu uungaji mkono kwa waathirika wa utumiaji nguvu wa ngono na jinsia – SGBV. Tunatafuta uwezo wa fedha ili kumalizia ujenzi wa hospitali ya uzazi katika mji mkuu Kinshasa ambayo itatowa pia ushauri nasaha kwa waathirika wa utumiaji nguvu wa ngono na jinsia pamoja na kutibu matatizo ya sehemu za siri za wagonjwa waathirika wa utumiaji nguvu wa ngono. Katika jimbo la Kivu Kusini, tunatafuta fedha za kugharimia miradi miwili: Ujenzi wa shule moja ya msingi, ambapo wanafunzi wake watakuwa watoto yatima ambaao wazazi wao wamekufa au wameathirika kwa virusi vya ukimwi au ugonjwa kamili wa ukimwi au watoto ambaao mama zao wameathirika na utumiaji nguvu wa ngono na jinsia – SGBV; na mradi mwingine wa hospitali kuu katika mji wa Wolungu ambayo itahudumia idadi kubwa ya wagonjwa katika maeneo ya mashambani ambaao ni pamoja na waathirika wa utumiaji nguvu wa ngono na jinsia.

Kudumisha Ushirikiano wa Nchi na Nchi, Utambuzi wa Hali na Uwezo wa Utendaji

Hali ya ushirikiano inazidi kukuwa kwa nguvu sana mionganoni mwa nchi za Afrika. Katika miaka miwili iliyopita, ushirika wa nchi za Afrika uliongezeka katika shughuli mbali mbali za eneo hilo la Afrika. Shughuli zetu zote zinataka kutumia hali hii ya ushirikiano ya kuzileta nchi washirika katika kujenga suluhisho la pamoja katika kukabiliana na changamoto katika swala la usalama. Shughuli zifuatazo ni muhimu katika kuonyesha sisitizo lake katika swala la utendaji.

Zoezi JITIHADA AFRIKA

Zoezi JITIHADA AFRIKA ni zoezi kabambe la utendaji katika sekta ya mawasiliano ambalo linahusisha idadi kubwa sana ya nchi washirika, na linaendelea kukuwa. Zoezi JITIHADA AFRIKA 09 nchini Gabon lilikusanya nchi 25 pamoja na mashirika matatu ya nchi za Afrika (Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi – ECOWAS, na Jumuiya ya Kiuchumi ya nchi za Afrika ya Kati). Likizingatia swala la kushirikisha habari mionganoni mwa nchi za Afrika kwa kupitia njia za mawasiliano, zoezi hilo liliunda ushirikiano wa mawasiliano na Marekani na Ushirika wa Kijeshi wa NATO, na nchi nyingine zenye ushwari wa kawaida, usalama, na malengo ya uendelezi katika eneo la Afrika. Washirika katika zoezi la mwaka 2010 la JITIHADA AFRIKA nchini Ghana wanatazamiwa kutoka nchi 30 za Afrika.

Zoezi PHOENIX EXPRESS, Afrika Kaskazini

PHOENIX EXPRESS ni zoezi la kimataifa la usalama baharini ambalo linaongozwa na jeshi la majini la Marekani, U.S. NAVAF na linazingatia ilani na marufuku baharini, mawasiliano na ushirikiano wa habari. Algeria, Libya, Morocco, na Tunisia ziliongeza ushiriki wake katika zoezi hilo mwaka jana.

Kufanya Kazi na Washirika dhidi ya Mapambano ya Kimataifa na Vitisho vya Siasa Kali

Changamoto za kimataifa katika bara la Afrika ni kitisho kwa Marekani, washirika wetu Afrika, na nchi washirika wa Marekani. Vitisho vya kimataifa ni vitisho ambavyo vinasababisha hali ngumu kwa wakazi wa nchi na kuleta ugumu katika juhudzi za kuleta mazingira ya usalama na ushwari yenye kutakiwa katika maendeleo. Sisi tunaendesha operesheni na ujenzi wa uwezo katika mipango na shughuli ambazo zinakabiliana na vitisho vya ugaidi, uharamia, biashara haramu ya dawa za kulevya na biashara nyingine za usafirishaji haramu.

Juhudi za Kupambana na ugaidi Afrika ya Kati na eneo la Sahel – OPERESHENI UDUMISHAJI UHURU- ENEO LA SAHARA (OEF-TS)

Kikosi Maalumu cha Operesheni Afrika (SOCAFRICA) kinaendesha shughuli za OEF-TS katika kupambana na vitisho vya kigaidi katika Afrika ya Kaskazini na Afrika Magharibi. OEF-TS inaunga mkono ushirikiano wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani katika ushirika wa eneo la Sahara wa kupambana na ugaidi (TSCTP) kwa kuzidisha uwezo wa washirika wetu wa kuzuia utowaji wa hifadhi kwa magaidi, kuimarisha usalama mipakani, kuhimiza utawala bora wa kidemokrasia, na kuhimiza uhusiano wa nchi za Afrika pamoja na ushirikiano wa kijeshi wa nchi na nchi. Shughuli za OEF-TS zimelelenga kuzimisha shughuli za vyama na makundi yenye siasa kali yenye kutumia nguvu katika bara zima la Afrika.

Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani na Balozi za Marekani ili kuhakikisha kwamba tunatowa msaada wa kijeshi wenyewe kuhitajika katika kutimiza malengo ya TSCTP, pamoja nayo ikiwa na haya yafuatayo: Operesheni za habari; mafunzo, ushauri na shughuli za misaada; uwezo katika swala la ujenzi wa upeletezi; maendeleo ya ushirikiano; mipango ya mazoezi ya kijeshi; na maendeleo na uundaji wa ushirikiano wa habari katika sekta ya komputa katika bara la Afrika. Shughuli zote za OEF-TS zinaratibiwa kwa ushirikiano na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani na timu za maafisa wa balozi zetu za Marekani katika nchi za Afrika.

SOCAFRICA ilibakia na nguvu ikiwa na shughuli nyingi sana mwaka jana na OEF-TS. Timu ya utowaji habari za kijeshi alisaidia juhudzi za diplomasia ya umma za Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani katika kupambana na nadharia ya makundi yenyeye siasa kali nchini Mauritania, Mali, Niger, Chad na Nigeria. OEF-TS ilianzisha uwezo wa mawasilliano ya Radio Kimkakati ya masafa ya juu kati ya Algeria na Niger. Na timu zenye kusafiri safari yenyeye kutowa mafunzo (MTT) zilitowa mafunzo kwa vikosi vipyta vyenye silaha ndogo ndogo vyenye kupambana na ugaidi nchini Mali. MTT vile vile ilitowa mafunzo kwa vikosi vya kupambana na ugaidi nchini Tunisi, Morocco, Nigeria, na Senegal. Mafunzo ya upeletezi jeshini yenyeye kutolewa na OEF-TS yalitolewa kwa wanafunzi kutoka nchi 7 za OET-TS, na mkutano wa usalama katika eneo la Sahara uliendesha mafunzo ya raia na wanajeshi karibu mia moja kutoka nchi 4 wa nchi washirika wa OEF-TS. Zaidi ya hivyo, idara za OEF-TS zinazoshughulikia raia na wanajeshi zilimaliza au zinapanga miradi 79 ya misaada ya kibinadamu.

Katika mwaka mmoja uliopita, hali ya kisiasa imeturuhusu sisi kurudia uhusiano wetu na Mauritania, na kujumuisha juhudzi zetu za kuunda kikosi cha kupambana na ugaidi. Majeshi ya usalama ya Mauritania yanakosa uwezo wa ugavi na usafirishaji kuweza kujiendesha wenyewe wakati wa operesheni. Kuisaidia Mauritania kujenga uwezo wa ugavi na usafirishaji kutasaidia majeshi ya usalama ya Mauritania kuwa na uwezo wa kupeleka wanajeshi wake na vifaa kwa vikosi vyake vilivyo mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya magaidi, vikosi ambavyo vinashughulika umbali wa maili mia kadhaa nje katika maeneo ya hali ngumu sana. Kwa kuititia misaada wa Marekani, Mauritania itakuwa na uwezo wa kudumisha operesheni zake za kijeshi katika mipaka yake na kwa ushirika wake na majeshi ya nchi nyiningine.

Katika Afrika Magharibi, tunajenga juhudzi zetu nchini Mali, Nigeria, Senegal na Burkina Faso. Shughuli zetu ni pamoja na mafunzo na kutowa vifaa kwa vikosi maalumu vyenye kupambana na ugaidi pamoja na kuzidisha uwezo wa upeletezi wa kijeshi na upashirikishaji wa habari katika kuunga mkono juhudzi za kupambana na nadharia za siasa kali katika eneo hilo la Afrika. Sisi tunafanya kazi na Mali kujenga uwezo wa kuboresha magari na vifaa, na kuimarisha usafiri wa angani, upeletezi, na uwezo wa ulinzi wa doria. Mipango hii miwili itaimarisha uwezo wa majeshi ya ulinzi ya Mali kuchukuwa hatua dhidi ya AQIM.

Juhudi za Kupambana na Ugaidi katika Afrika ya Mashariki

Katika Afrika ya Mashariki, Kundi maalumu CJTF-HOA liliopo chini ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika linaendesha operesheni za kupambana na makundi yenye siasa kali yenye kutumia nguvu katika eneo zima ili kulinda maslahi ya Marekani na nchi washirika wa Marekani. Kwa ushirikiano na wizara na idara za serekali ya Marekani, CJTF-HOA inazingatia operesheni zake katika kujenga uwezo wa usalama katika nchi za Afrika Mashariki ili kupambana na ugaidi, kuzuia hifadhi kwa magaidi, na kupunguza misaada yenye kupatiwa makundi yenye siasa kali. CJTF-HOA linatekeleza malengo yake kuititia timu za maafisa wa maswala ya kiraia, timu za ujenzi za “Seabee”, washauri wa kijeshi, na kwa kuingiza masomo ya usalama na ulinzi.

Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kimezingatia shughuli zake nyingi za uwezo wa mapambano dhidi ya ugaidi katika Afrika ya Mashariki, nchini Kenya, Ethiopia, Djibouti, na Uganda, nchi ambazo- mbali na Somalia, ni nchi ambazo zitatishiwa moja kwa moja na magaidi. Kwa mfano, nchini Kenya, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinasaidia kuunda kikosi cha mapambano, Ranger Strike Force, na kikosi maalumu cha jeshi lenye kutumia boti ambalo litakuwa hatimaye majeshi ya kupambana na ugaidi na usalama wa mipakani. SOCAFRICA lilimaliza mafunzo ya kombania mbili za jeshi la mashambulio, Kenya Ranger Strike Force, na juhudi za majeshi yetu maalumu ya operesheni (SOF) baharini yameanzisha kikosi maalumu cha wanajeshi wenyе kutumia boti ili kuzidisha uwezo wa usalama wa baharini wa Kenya. Wakati miradi yote hii ikimalizika kuundwa, Kenya itakuwa imeimarisha uwezo wake sana wa kupambana na kitisho cha ugaidi wenyе kutokea Somalia.

Nchini Djibouti, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinasaidia kutowa mafunzo kwa kikosi cha kupambana na ugaidi, Groupe d’Intervention de la Gendarmerie Nationale. Tunasaidia kuboresha na kuhamisha magari 12 kutoka Umoja wa Afrika na kuyafikisha Djibouti. Magari hayo yatatumiwa katika shughuli za kupambana na ugaidi na usalama wa mipakani.

Jeshi la Uganda, Uganda People’s Defence Forces, (UPDF) ni moja ya majeshi ya kitaalamu katika eneo la Afrika ya Mashariki. Ni jeshi shirika katika mapambano dhidi ya ugaidi kwa ushirikiano na washirika wa eneo hilo la Afrika, na linaongoza operesheni dhidi ya waasi wa Lord’s Resistance Army. Jeshi la kulinda amani la Uganda nchini Somalia lime tekeleza jukumu kubwa muhimu katika kuipa serikali ya mpito ya Somalia (TFG) fursa ya kujijenga. Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika na CJTF-HOA vinaendelea kufanya kazi na jeshi la Wananchi la Uganda UPDF ili kuzidisha uwezo wa kulinda amani na uwezo wa CT kwa kuititia msaada wa mafunzo wa operesheni Afrika (ACOTA), IMET, na mafunzo yenye kugharimiwa na PKO.

Mipango ya Kupambana na Biashara za Dawa za Kulevyta

Mipango yetu ya kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevyta inatowa mafunzo, inatowa vifaa, na kuunga mkono majeshi ya taifa ya kutekeleza sheria, vikosi vya kijeshi na polisi vyenye misheni za kupambana na biashara hiyo haramu ya dawa za kulevyta. Mipango hiyo inajenga uwezo wa washirika na kuwezesha kuendeshwa kwa shughuli kamili za kupambana na dawa za kulevyta, kama vile kushirikisha habari, kugunduwa vitisho na kuingilia kati na kukamata vyombo vya usafiri vyenye kutumiwa.

Moja ya mafanikio katika mwaka uliopita ilikuwa katika ujenzi wa kituo kipyta cha kimataifa cha idara mbali mbali katika taifa la Cape Verde, ujenzi ambaa uligharimiwa na idara ya kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevyta. Kituo hicho kinashirikisha majeshi ya kutekeleza sheria ya Marekani, Polisi wa Kimataifa, na idara mbali mbali za kutekeleza sheria za Cape Verde na majeshi ya baharini, na miradi ya Marekani ya FMS yatatowa vyombo vya usafiri wa baharini. Jeshi letu la majini pamoja na jeshi la ulinzi wa pwani ya Marekani yanatowa mafunzo ya ubaharia. Idara ya Marekani yenye kupambana na madawa haramu, Wizara ya Ulinzi ya Marekani, na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani ni wachangiaji wakubwa. Lengo ni kujenga jeshi la baharini nchini Cape Verde lenye uwezo wa kugunduwa na kukamata wafanyabiashara haramu, na kushirikisha habari muhimu sana na idara za usalama za Marekani na jamii ya kimataifa.

Operesheni SAUTI YENYE LENGO (OOV)

OOV ni operesheni ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika katika juhudi yake ya kukabiliana na siasa kali zenyetutu kutumia nguvu kwa kuhimiza uwezo wa vyombo vya habari kwa njia ambayo inahimiza umma kipinga nadharia za siasa kali. OOV inashirikiana sana na Balozi za Marekani, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Wizara ya Marekani inayoshughulikia Maendeleo ya Kimataifa (USAID), na inatumia majukwaa mbali mbali katika kipeleka ujumbe wake, kama vile Shinikizo la Mtandao Afrika, kukabiliana na maoni ya makundi ya kigaidi na kutowa jukwaa kwa watu kuelezea maoni yao tofauti. OOV vile vile, huunga mkono juhudi za ndani ya nchi za kudumisha amani, uvumilivu na ufahamu. Mifano ni pamoja na michezo ya “amani kwa vijana” nchini Mali na mradi wa filamu Kaskazini mwa Nigeria. Ushahidi wa kweli unaonyesha kwamba mijadala yenye kuhimizwa imekuwa na athari bora. Sisi hivi sasa tunakusanya takwimu za kimsingi na kujenga makadirio na tathimini ya athari ya jumla ya hatua zetu.

Kuchangia Ushwari katika Maeneo ya Migogoro hivi sasa

Juhudi za muda mrefu za kujenga uwezo wa usalama zinaweza kufaulu katika mazingira yenye ushwari wa kutosha. Marekani inaunga mkono juhudi za Afrika za kuleta ushwari katika maeneo ya migogoro ya hivi sasa na inayoweza kutokea baadaye kwa kutumia misheni za

kulinda amani na kuimarisha uwezo wa kulinda amani ambao unajumuisha juhudzi za jeshi la tahadhari la Umoja wa Afrika.

Sudan

Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinafanya kazi kwa uhusiano wa karibu na wahuksika katika serikali ya Marekani kuunga mkono utekelezaji wa mkakati mkubwa wa Marekani katika Sudan. Katika Kusini mwa Sudan, Kikosi hicho kinaunga mkono elimu kwa jeshi lenye utaalamu na kwa maafisa wasiofuzu katika upande wa maendeleo, mafunzo na semina kuhusu virusi vya ukimwi na ugonjwa wa ukimwi (HIV/AIDS), pamoja na matukio ya utambulisho kwa ujuzi wa kijeshi na utekelezaji. Zaidi ya hivyo, tunatathimini njia ambazo mali zetu na uwezo wetu unaweza kuimarisha misheni za Umoja wa Mataifa katika taifa, na jinsi gani sisi tunawenza kuendelea kusaidia juhudzi za mageuzi katika sekta ya usalama zenye kufanywa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani.

Somalia

Ukosefu wa serekali kuu yenye kutawala nchini Somalia kwa muda karibu miaka ishirini sasa umesababisha hali kubwa ya kuyumbisha nchini humo. Imeiacha nchi hiyo ikiyumbishwa na magaidi, na kuleta mazingira ya uharamia na shughuli nyingine haramu. Hali hiyo pia imesababisha maafa makubwa ya kibinadamu. AMISON, mishani ya Umoja wa Afrika nchini Somalia inakabiliwa na upungufu mkubwa wa uwezo, lakini ni mishani muhimu sana kwa usalama katika maeneo ya TFG. Misaada ya Serikali ya Marekani kwa AMISOM ni pamoja na mafunzo, vifaa, na ugavi na usafirishaji kwa majeshi ya Uganda na Burundi. Zaidi ya hivyo, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinatowa wanajeshi wanaishi kwa ACOTA, mafunzo ya awali kwa majeshi ya AMISOM kabla ya kupelekwa Somalia . kabla ya kupelekwa, kila kombania inapata mafunzo na ujuzi wa kijeshi ambao una msingi wa PKO na mazingira halisi ya operesheni za jeshi nchini Somalia.

Sisi vile vile tunaunga mkono operesheni za jeshi la Marekani katika kukabiliana na kuongezeka kwa uharamia magharibi ya bahari ya Hindi. Mafunzo ya kupambana na uharamia ni sehemu ya ujenzi wetu wa uwezo baharini katika nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika, kama vile Kituo cha Ushirika Afrika – Mashariki.

Juhudi za Kuendesha Operesheni za Kuleta Amani Duniani (GPOI)

Juhudi za Kuendesha Operesheni za Kuleta Amani Duniani (GPOI) ni mpango wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani ambao unajenga uwezo wa kudumisha amani

katika nchi washirika na mashirika ambayo yamelengwa. Mpango huo wa GPOI ambao unagharimiwa na ACOTA unaungwa mkono kwa kawaida na Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika na maafisa wake wa juu na wa chini ambao wanafanya kazi kama waaalimu na wanaasihi. ACOTA imefundisha na imetowa vifaa kwa majeshi ya Uganda na Burundi yaliyopo katika jeshi la kulinda amani Somalia, AMASOM, na imefundisha majeshi ya Rwanda, Afrika ya Kusini, Zambia, na Tanzania kwa niaba ya UNAMID.

Kwa mwaka wa fedha wa 2010, Kikosi cha Jeshi la Marekani Afrika kimeomba fedha kwa ajili ya juhudi za kuendesha operesheni za kuleta amani duniani (GPOI) ili kuunga mkono mipango ya mafunzo ya kuhimiza uwezo wa majeshi ya kulinda amani ya Umoja wa Afrika, Jumuia ya Kiuchumi ya nchi za Afrika Magharibi, Jumuia ya Kiuchumi ya nchi za Afrika ya Kati na makao makuu ya jeshi la tahadhari la Jumuia ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika. Tumeomba pia fedha za kugharimia shughuli za vikosi vya mikakati za nchi wanachama ambavyo ni majeshi ya tahadhari katika nchi za Afrika.

Kukabiliana na Hali ambayo Inachangia Uyumbishaji

Jeshi la Marekani lina mipango kadhaa ya kiraia na kijeshi ambayo inahimiza uhusiano mzuri wa raia na jeshi, unatowa faida za mafunzo ya kijeshi, na kusaidia kuunda uwezo katika maswala ya kibinadamu katika nchi za Afrika. Mipango hiyo inaunga mkono juhudi za maendeleo ya kiraia na inashirikishwa na kuratibiwa na timu ya maafisa wa ubalozi wa Marekani katika taifa.

Zoezi MEDFLAG

Augusti mwaka 2009, MEDFLAG 09 iliendeshwa kwa ushirikiano na jeshi la ulinzi la Umbutfo, nchini Swaziland kama zoezi la pamoja la uwezo wa tiba/meno/ na afya ya wanyama. Jeshi la Marekani Afrika na jeshi la angani la Marekani liliweka waathiriwa wa maafa halaiki ambao walisaidia kupima uwezo wa jeshi la ulinzi na uwezo wake wa kukabiliana na hatua za mwanzo za kusaidia majeruhi raia. Zoezi hilo lilisaidia wizara ya afya ya Swaziland na wizara ya ulinzi ya nchi hiyo kutathimini kwa pamoja mipango ya kukabiliana na maafa ya dharura na utaratibu wake. MEDFLAG 09 ilisaidia kuimarisha uwezo wa Swaziland wa kuunga mkono misheni za siku za mbele za Umoja wa Afrika na UN PKO, wakati tukiangazi uungaji wetu mkono katika eneo hili la bara la Afrika.

Mpango wa Kukabiliana na Magonjwa ya Halaiki

Kwa sababu magonjwa ya kuambukiza yana uwezo wa kuenea haraka na kuwa maafa kwa dunia mzima, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinafanya kazi na washirika wake wa nchi za Afrika, idara mbali mbali, mashirika ya kimataifa, na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) kujenga ushirika na uwezo wa kijeshi ili kukabiliana na magonjwa ya halaiki. Juhudi zetu zinaimarishwa na msaada wa fedha wa miaka mitatu kutoka Idara ya Marekani inayosughulikia maendeleo ya kimataifa (USAID), ambayo inashirikiana na Shirikisho la Kimataifa la Msalaba Mwekundu na chama cha Mwezi Mwekundu na mashirika mengine washiriki katika nchi za Afrika.

Mpango wa Kukabiliana na Virusi vya Ukimwi na Ugonjwa Kamili wa Ukimwi (HIV/AIDS)

Mpango wa Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika wa kukabiliana na virusi vya ukimwi na ugonjwa kamili wa ukimwi una lengo la kukabiliana na athari za ugonjwa huo dhidi ya uwezo wa kuwa tayari wa majeshi ya Afrika. Mpango huo ni pamoja na shughuli ambazo zinasaidia kuzuia kiwango cha maambukizo ya virusi vya ukimwi na ugonjwa kamili wa ukimwi (HIV/AIDS) katika majeshi ya ulinzi ya nchi za Afrika, na kutowa huduma na tiba kwa wanajeshi na familia zao ambao wameambukizwa na ugonjwa huu. Wizara ya Ulinzi ya Marekani shughuli zake ambazo zinaunga mkono mapambano ya majeshi ya Afrika dhidi ya ukimwi sasa zinazifikia nchi 39 za Afrika. Katika sehemu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2009, mipango ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika iliwafikia wanajeshi zaidi ya 117,000 Waafrika na familia zao na ujumbe wa kuzuia maambukizo, na kilitowa ushauri na kuwapima wanajeshi na familia zao wapatao 114,430. Zaidi ya hivyo, viongozi 111 wa ngazi ya juu jeshini wamefundishwa sera za virusi vya ukimwi na ugonjwa kamili wa ukimwi, na waalimu 2,396 pamoja na wafanyakazi 517 wa huduma za afya wamepatiwa mafunzo ya ugonjwa wa ukimwi. Zaidi ya watu 19,000 wanapatiwa tiba ya dawa mchanganyiko za ugonjwa wa ukimwi kutokana na juhudu hizo. Mapambano dhidi ya ugonjwa wa ukimwi katika Afrika yanaleta matokeo. Hivi karibuni kiongozi mmoja wa nchi katika Kusini mwa Afrika alitamka kwamba, miaka mitatu iliyopita alikuwa anaendesa mazishi kila siku kwa wagonjwa wa ukimwi; hii leo alisema, anaendesa mazishi ya mtu mmoja kila siku nane hadi kumi.

MAKUBALIANO YA KUSHIRIKIANA, Benin

Pale inapowezekana, sisi tunachanganya operesheni za kiraia na majeshi katika mazoezi yetu. MAKUBALIANO YA KUSHIRIKISHA ni mfano mmoja. Mazoezi yenye kuendeshwa na U.S. MARFORAF, MAKUBALIANO YA KUSHIRIKISHA lengo lake la msingi ni kutowa mafunzo ambayo yanaunga mkono operesheni za kulinda amani na udumishaji amani, na zoezi hilo kwa mafanikio liliunganisha kombania mbili za jeshi la ardhini la Benin na kombania mbili za jeshi la Marines la Marekani la ardhini. Zoezi zaidi lilikuwa zoezi la mpango wa huduma za kiraia za tiba na meno, zoezi ambalo lilitibu wagonjwa 7,370 katika ziara za kutembelea vijiji

vitatu katika muda wa siku nane. Mpango tofauti wa huduma kwa wanyama ulitibu wanyama 92,410 wakati wa ziara ya vijiji saba katika muda huo huo. Zoezi la ujenzi wa kuzidisha uwezo wa Benin wa kuendesha mafunzo ya ulinzi wa amani katika kituo cha mafunzo ya amani cha Bembereke lilitimizwa pia.

KIKOSI CHA JESHI LA MAREKANI AFRIKA NA IDARA ZAKE ZA CHINI

Kikosi cha Jeshi la Marekani Afrika idara nne chini yake, idara moja ambayo imejumuishwa na jeshi la pamoja katika Pembe ya Afrika. Idara zetu zimeanzishwa karibuni tu na zimerithi juhudhi za awali ambazo ni lazima zifuate mkakati wa Kikosi cha Jeshi la Marekani Afrika. Idara za Kikosi cha Jeshi la Marekani Afrika na idara za chini yake ni watekelezaji wa mipango yetu na shughuli zetu katika bara la Afrika. Kwa vile idara zetu hazina majeshi yaliyopewa, sisi tunategemea kupata wanajeshi wanaoidhinishwa na Wizara ya Ulinzi ya Marekani kwa ajili ya uwezo ambao tunauhitaji katika kuendesha majukumu yetu katika Afrika.

Jeshi la Ardhini la Marekani (USARAF)

Octoba mosi, mwaka 2009, Waziri wa Jeshi la Ardhini wa Marekani alilitowa jeshi la ardhini la Marekani katika Afrika (ASCC) kuwa sehemu ya jeshi chini ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika. Jeshi la Ardhini la Marekani USARAF litakuwa kamilifu kama Jeshi la Ardhini la Marekani katika Afrika katika mwaka wa fedha wa 2012. Jeshi hilo limeongezeka mara mbili katika muda wa miezi 15 iliyopita. USARAF inaendelea kujishughulisha sana na maendeleo ya kitalaamu ya majeshi ya ardhini ya Afrika, ambayo yanabakia kuwa majeshi yenye kutegemewa katika nchi nyingi za Afrika. Lengo la USARAF ni kusaidia kuyageuza majeshi ya ardhini ya washirika wetu kuwa wachangiaji wa amani na ushwari, yakiwa na uwezo wa nafasi zenyenye kutakiwa katika kutimiza misheni zao za kuunga mkono utawala halali.

USARAF inaendelea kutafuta uhusiano wa ushirikiano na kudumisha uhusiano ambao unachangia kuleta uwezo wa kiusalama na ulinzi wenye kuendelezwa na nchi za Afrika. Sababu kuu ya mafanikio ya USARAF ni ushirikiano wake na washirika wake wa kijeshi na wasio wa kijeshi. USARAF inadumisha uhusiano mpya na kuhimiza uhusiano uliopo, na kujumuisha uhusiano na idara nyingine za serikali ya Marekani.

Zoezi liitwalo MOTO ASILIA liligharimiwa na kuendesha na USARAF, zoezi kubwa kabisa katika bara la Afrika lilofanyika mwaka jana. Zoezi hilo liliunganisha majeshi ya Marekani kutoka Ulaya na Marekani na wanajeshi wake walijiunga na majeshi kutoka nchi tano za Afrika na kuzingatia zoezi la misaada ya kibinadamu na huduma wakati wa maafa. Lilifanyika nchini Uganda.

Majeshi ya Majini ya Marekani, Afrika (NAVAF)

Misheni ya NAVAFA kimsingi ni kuimarisha uwezo wa kudumisha usalama baharini wa washirika wetu wa bara la Afrika. Mbali na APS, na operesheni za majeshi ya kutekeleza sheria, na shughuli za ushirikiano wa usalama, NAVAFA inafanya kazi kuhimiza usalama wa baharini kwa kuzingatia maendeleo ya ufahamu wa shughuli za baharini, mafunzo kwa watalaamu, na miuindombinu ya baharini, uwezo wa kujibisha matokeo, ushirika kati ya nchi na nchi, na mtazamo thabiti wa upangaji mipango na utekelezaji wake. Uwezo huo utaimarisha usalama wa baharini na kuchangia maendeleo na ushwari kwa kuruhusu washirika wetu kutumia fursa ya uwezo uliopo katika maeneo yao ya kiuchumi.

NAVAF, ambayo makao yake yapo Napoli, nchini Italia, inaunga mkono kuwepo kwa mazingira ambayo nchi zote za Afrika zitakuwa na haja ya kuwa na usalama wake wa baharini na katika usalama wa eneo zima la Afrika. NAVAFA hutumia shughuli zake za baharini katika kujenga imani, ushirikiano wa pamoja na heshima, ili kuweza kulinda maslahi ya Marekani, kupunguza mahitaji dhidi ya uwezo wa fedha wa Marekani, na kuhakikisha kuna nafasi na fursa za kuaminika katika bandari, na maeneo ya bahari yenye kumilikiwa na mataifa na mahitaji mengine ambayo yanatakiwa katika kuendeleza shughuli za safari za baharini.

Jeshi la Angani la Marekani, Afrika (AFAFRICA/17AF)

Kikosi cha 17 cha jeshi la angani la Marekani ni sehemu ya jeshi la angani la Marekani lililopo chini ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika. AFAFRICA ni jeshi linaloendelea kukuwa katika uwezo wake wa kumudu na kudhibiti majeshi ya angani ya nchi za Afrika kwa madhumuni ya kuendeleza operesheni na shughuli za usalama, na kuhimiza maendeleo, usalama angani na ulinzi.

AFAFRICA imejengwa na wanajeshi wa jeshi la angani la wanajeshi (AFFOR) na Kituo cha 617 cha operesheni za angani na anga ya juu (AOC). Watumishi wa AFFOR wa AFAFRICA walifikia FOC October mosi, mwaka 2009. AOC 617 inatazamiwa kutimiza FOC Juni mosi, mwaka 2010. AOC hutowa huduma na udhibiti wa angani kwa mazoezi yote ya usalama wa angani pamoja na kutowa huduma kama vile misaada ya kibinadamu nchi za nje na operesheni za kuhamisha watu katika mazingira yasiyo na mapigano. Makao yake yakiwa katika kituo cha Jeshi la Angani la Marekani mjini Ramstein, Ujeruman, wafanyakazi wake mia tatu wapo chini ya jeshi la angani la Marekani katika Ulaya na inagharimiwa na Wizara ya Ulinzi ya Marekani. AFAFRICA inawajibika kwa Kikosi Maalummu cha Jeshi la Marekani Afrika kwa operesheni zake zote na uungaji mkono wa pamoja.

Moja ya shughuli kubwa za AFAFRICA ni Usalama wa Angani na Ulinzi (ADSS) mpango ambao ni wa muda mrefu wa jeshi la angani la Marekani ambapo mfuko wake wa fedha za matumizi kwa mwaka wa fedha wa mwaka 2010 ni dola za Marekani milioni 2.6. Mfuko huo

wa fedha unatazamiwa kupanda hadi kufikia dola milioni 3.1 katika mwaka wa fedha wa mwaka 2011. AFAFRICA itapanuwa shughuli za usalama na ulinzi wa angani (ADSS) kwa kiasi kikubwa katika mwaka huu wa 2010 kwa kuyatumia majeshi ya angani ya majukumu ya jumla na kufanya kazi kwa pamoja na idara na wizara za serikali ya Marekani na washirika wengine katika kujenga na kuendeleza uwezo wa nchi za Afrika wa kudumisha usalama na ulinzi wa angani kwa shughuli za kiraia na kijeshi angani. Majadiliano na Rwanda, Uganda, Nigeria, na Ghana yamo njiani, na yataweka msingi wa hali halisi ya shughuli za angani katika Afrika.

Majeshi ya Marines ya Marekani, Afrika (MARFORAF)

MARFORAF yenyе makao yake mjini Stuttgart, Ujerumanı, huendesha operesheni zake, mazoezi, mafunzo, na ushirikiano wa shughuli za usalama kote katika AOR. Katika mwaka 2009, MARFORAF ilishiriki katika misheni 15 za ACOTA ambazo zilikuwa na lengo la kuimarisha uwezo wa nchi washirika na kutowa msaada wa ugavi na usafirishaji, kutumia polisi wa kijeshi, na kutekeleza mamlaka na udhibiti dhidi ya majeshi ambayo yamepelekwa vitani au shughuli nyingine. Kama mjambe mkuu mtendaji wa mpango wa silaha zisizokuwa za mashambulizi makubwa, MARFORAF iliendesha zoezi lenye mafanikio makubwa ambalo lilihudhuriwa na nchi 11 za Afrika. Zoezi hilo lilionyesha aina nyingi za silaha ambazo zinaweza kuzuia kuenea kwa vitendo vya utumiaji nguvu na kuongeza uwezo wa mikakati ya kiongozi wa jeshi katika kudhibiti hali bila ya kutumia silaha kali.

MARFORAF iliendesha matukio mengi katika mwaka 2009 ambayo yalinuiwa kuwatambulisha washirika wetu wa Afrika karibu kila aina ya operesheni za kijeshi na utaratibu wake, pamoja nao ikiwa ni matumizi ya vyombo vya angani, mikakati na ujuzi wa tiba. MARFORAF, ikiwa ni chombo chenye kuongoza, inaendelea kuendesha zoezi LA SIMBA WA AFRIKA nchini Morocco -- zoezi kubwa kabisa la kila mwaka lenye kujumuisha Wakuu wa majeshi katika bara la Afrika pamoja na zoezi la MAKUBALIANO YA KUSHIRIKISHA 10, ambayo yatakuwa ya kwanza ya CJCS kufanyika nchini Msumbiji.

Mamlaka Maalumu ya Operesheni za Jeshi la Marekani, Afrika (SOCAFRICA)

Octoba mosi mwaka 2008, SOCAFRICA iliundwa kama sehemu ya Majeshi Maalumu ya Operesheni (SOF) ya utendaji ya chini ya mamlaka ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani. SOCAFRICA makao yake yamewekwa pamoja na Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika katika kambi ya jeshi ya Kelley, Stuttgart, nchini Ujerumanı.

Vile vile, Octoba Mosi mwaka 2008, SOCAFRICA ilichukuwa madaraka ya kuendesha Operesheni Maalumu na Udhibiti katika Pembe ya Afrika, na Mei 15 mwaka 2009, SOCAFRICA ilichukuwa madaraka ya Operesheni Maalumu za Pamoja katika eneo la Sahara (JSOTF-TS) – sehemu ya SOF ya Operesheni Dumisha Uhuru – katika eneo la Sahara.

SOCAFRICA malengo yake ni ujezni wa uwezo wa kuendesha operesheni, kuimarisha usalama katika Afrika na kuleta juhudzi za uwezo, kutekeleza mikakati yenyeye ufanisi ya mawasiliano katika kuunga mkono malengo ya kimkakati, na kuyazima makundi yenyeye siasa kali yenyeye kutumia nguvu pamoja na kuzimisha misaada yake. Majeshi ya SOCAFRICA hufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na ubalozi wa Marekani katika taifa na washirika Waafrika, ikidumisha idadi ndogo yenyeye uwezo katika Afrika mzima, hasa hasa katika maeneo ya OEF-TS na CJTF. SOCAFRICA sisitizo lake la kuwepo kwa SOF linatowa uwezo mkubwa ambao unaunga mkono juhudzi za serikali ya Marekani ya kupambana na makundi yenyeye siasa kali yenyeye kutumia nguvu na kujenga uwezo wa taifa wa CT.

Jeshi la Pamoja la Marekani katika Pembe ya Afrika (CJTF-HOA)

Katika Afrika Mashariki na Afrika ya Kati, CJTF-HOA ni muhimu sana kwa Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika katika juhudzi zake za kujenga uwezo wa washirika wake katika kukabiliana na makundi yenyeye siasa kali yenyeye kutumia nguvu na kukabiliana na changamoto nyingine za usalama katika eneo hilo la Afrika. Mishani yake ya kukabiliana na makundi yenyeye siasa kali yenyeye kutumia nguvu na makao yake katika kambi ya Lemonnier inabakia kuwa muhimu sana hasa tukichukulia ukweli kwamba vitisho katika eneo hilo la Afrika kutoka kwa al-Qaeda na al-Shabaab nchini Somalia na al-Qaeda nchini Yemen. Ili kukabiliana na makundi yenyeye siasa kali, CJTF-HOA hufanya kazi kwa njia kadhaa:

Kudumisha Ushirikiano wa nchi na nchi katika swala la Usalama: CJTF-HOA hufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na wanachama washirika katika Ulaya, nchi washirika katika Afrika, na Wizara na Idara mbali mbali za serekali ya Marekani, na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) ambayo yanashughulika katika eneo la operesheni za pamoja. CJTF-HOA inadumisha ushirikiano katika mambo ya usalama na nchi za Afrika kwa kuititia uungaji mkono wa jeshi la tahadhari la Afrika ya Mashariki, kituo cha mafunzo ya ulinzi wa usalama wa kimataifa, chuo cha amani ya kibinadamu, ACOTA, Jumuia ya Afrika ya Mashariki, na mazoezi ya Afrika Mashariki ya kujitayarisha kwa maafa katika maeneo ya Afrika, mazoezi kama vile MOTO ASILI na MKUKI WA DHAHABU.

Kuimarisha Uwezo wa Washirika katika Usalama wa Taifa: Operesheni za kiraia na kijeshi, shughuli, na mipango ya maendeleo hutowa kwa Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika njia mbali mbali za kuimarisha uwezo wa shughuli za usalama kwa nchi mshiriki. Timu za maafisa wa kiraia husaidia washirika wetu kuhimiza uhalali wa serikali zao na majeshi yao. Kwa ushirikiano na Idara ya Marekani ya Maendeleo ya Kimataifa (USAID) na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, shughuli za kiraia zinasaidia kuondowa matatizo ambayo yanaweza kuchangia katika uyumbishaji wa nchi hizo za Afrika. CJTF-HOA vile vile inaimarisha uwezo wa usalama wan chi washirika kwa kuunga mkono APS; kutowa fursa kwa majeshi washirika wetu Waafrika kuweza kufanya kazi kwa karibu na timu za CA; kujenga uwezo wa usalama na ulinzi na kupambana na uharamia; na kwa kutowa fursa kwa maafisa waratibu wa kijeshi

kutumika katika CJTF-HOA. Uungaji mkono wa CJTF-HOA nchini Djibouti katika kutowa mafunzo kwa wanajeshi wa TFG wa Somalia na kuunga mkono mazoezi na mafunzo ya majeshi ya tahadhari ya Afrika ya Mashariki umeimarisha uwezo wa taifa la Djibouti wa kuchukuwa jukumu kubwa katika kudumisha na kuhimiza amani katika Pembe ya Africa.

WAWEZESHAJI MAENDESHO: CHANGAMOTO NA FURSA

Upana na uzito wa mipango ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika na shughuli zake katika Afrika ni mambo yenye kuongezeka na kukuwa sana. Uwezo wetu wa kuendeleza mbele maendeleo ya kufikia malengo yetu ya muda mrefu katika Afrika yanategemea mambo kadhaa ambayo yanaruhusu juhudhi zetu. Baadhi yake, kama vile mipaka ya mamlaka, ni mambo ambayo yanatuletea changamoto pale tunapotafuta msaada. Mengine, ni kama vile uunganishaji wa shughuli za idara mbali mbali, mambo ambayo yanaleta fursa ya kupanua na kuendelea kwa mipango mipya au ilioimariswa na shughuli ambazo sisi tunataka kuziendeleza.

Mamlaka

Kuendeleza mipango yetu ya muda mrefu ya ushirikiano wa usalama na shughuli zetu katika Afrika kunahitaji mamlaka yasiyo na kipingamizi na miaka mingi. Mamlaka iliyopo sasa imenuiwa kuunga mkono shughuli binafsi za muda mfupi au muda mrefu, lakini haziungi mkono shughuli za zamani na za sasa. Vile vile, mamlaka hayo hayatoshi katika utekelezaji wa mambo katika hali ambayo inabadilika, kama vile wakati juhudhi za kutowa mafunzo na vifaa zenye kutokana na kutokea kwa vitisho ambavyo vinaonyesha haja ya kuwa na ujenzi wa uwezo wa muda mrefu.

Mamlaka na mipango ambayo sisi tunaitumia hivi sasa kwa kujenga uwezo wa washirika wetu ni muhimu na mimi naomba uungaji wenu mkono wenyewe kuendelea katika maeneo yafuatayo:

- Uungaji mkono kamilifu wa maombi ya bajeti yaliyotolewa na rais kwa ajili ya mpango wa mafunzo na vifaa
- Uungaji mkono wa maombi ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje kwa ajili ya mipango katika Afrika
- Uungaji mkono wa mfuko wa fedha kwa ajili ya Makamanda katika uwanja wa mapambano, kukitolewa uhuru wa kutolewa shughuli za elimu na mafunzo kwa majeshi ya nchi za nje

Tunahimiza kuwepo kwa mjadala kujadili njia za kupunguza au kurekebisha mamlaka ya sheria ili kuwezesha shughulli za kudumisha usalama na washirika wetu wa Afrika, kuanzia

swala la mafunzo na mipango ya vifaa mambo ambayo yanakabiliwa na mabadiliko ya haraka katika ujenzi wa uwezo wa muda mrefu, na hasa katika swala la kupambana na makundi yenye siasa kali yenye kutumia nguvu.

Miundombinu na Mahitaji Halisi

Miundombinu ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika ilirithiwa na mamlaka tatu zilizopita ambazo zilikuwa na majukumu ya Wizara ya Ulinzi ya Marekani kwa Afrika. Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani kinatathini na kusawazisha haja zake za maendesho na mahitaji yake kote ambako kinashughulika katika Afrika. Swala zima linahusu kupata na kudumisha uwezo wa maendesho na uhuru wa kusafiri kuendesha shughuli za ushirikiano wa usalama, na kama ikihitajika, operesheni za kukabiliana na maafa. Tunafanya kazi na wenzetu katika ofisi ya Waziri wa Ulinzi, na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani ili kutambulisha sehemu za ushirikiano wa usalama (CSLs) na kuunga mkono makubaliano yenye kuhitajika ili kuwezesha Kikosi cha Jeshi Maalumu la Marekani Afrika kuendesha shughuli hizi. Hivi sasa sehemu kumi za ushirikiano wa usalama zimekwisha tambuliwa, nane kati yake zilikuwa zimeanzishwa na mamlaka ya jeshi la Marekani katika Ulaya na mamlaka makuu ya majeshi ya Marekani eneo la kati. Mipango mikuu ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika mpango wake na uwezo wake vimenuwa kukabiliana na mahitaji yenye kutokeza ya uungaji mkono.

Vituo vya Operesheni za Mbele (FOS) na Vituo vya Ushirikiano wa Usalama vya AOR katika Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika

Kambi ya Lemonnier nchini Djibouti (CLDJ) ni kituo muhimu sana kwa maslahi ya usalama ya Marekani katika Afrika ya Mashariki na eneo zima la bahari ya Hindi. Kituo hiki kinaunga mkono juhudzi zenyet kufanyika katika ghuba ya Aden pamoja na malengo ya mamlaka makuu ya majeshi ya Marekani eneo la kati katika taifa la Yemen. Kambi hiyo ikiwa inapakana na uwanja wa ndege wa Djibouti na ukaribu wake na bandari ya Djibouti unaifanya kambi hiyo ya Lemonnier (CLDJ) kuwa ya manufaa katika kuunga mkono operesheni za Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika katika eneo zima la Afrika, na umuhimu sawa kwa uwezo wa kambi hiyo kuunga mkono miundombinu ya ufafirishaji duniani kote wa Wizara ya Ulinzi ya Marekani. Kambi ya Lemonnier inaunga mkono pia washirika wetu duniani wakati tunafanya kazi ya kupambana na uharamia wa baharini katika Afrika.

Tunaibadilisha kambi hiyo (CLDJ) kutoka hali yake ya zamani na kujenga upya kambi ya kudumu ambayo inagharimiwa na mpango wa ujenzi wa jeshi. Miradi ya mwanzo itaimarisha usalama na ulinzi. Miradi itakayofuatia itaimarisha uwezo wa operesheni wa kuendelezwa.

Kituo cha pili cha FOS, kipo katika kisiwa cha Ascension, nacho pia, ni kituo muhimu sana kwa usafirishaji katika kuunga mkono shughuli za Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani

Afrika – na kupanua operesheni zetu ili kuzifikia nchi za Afrika Magharibi na Kusini mwa Afrika. Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinafanya kazi na jeshi la usafirishaji la Marekani katika kuunda miundombinu ya kituo hiki cha FOS ili kiweze kuunga mkono zaidi shughuli za Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika.

Kupitia miundombinu ya nje ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika – AOR

Zaidi ya miundombinu ya ufasirishaji ndani ya AOR, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kinaendelea kutegemea vituo vya pembeni na kambi za kuendeshea operesheni katika mji wa Rota nchini Uhispainia, Sigonela, Italia, Aruba (Lesser Antilles), Souda Bay Ugoriki, na Ramstein nchini Ujerumani kwa maswala ya ugavi na usafirishaji. Ingawaje vituo hivi vipo katika eneo lingine la mamlaka ya AOR kijografia, ni vituo muhimu sana vyenye kuunga mkono operesheni zetu katika bara la Afrika.

Mamlaka, Udhibiti, Mawasiliano, na miundombinu ya mfumo wa komputa (C4S)

Yote hapo juu yanaelekeza katika mahitaji ya kuwepo uwekezaji mkubwa sana katika kujenga uwezo wa miundombinu ya mfumo wa komputa C4S katika vituo vyetu vya kambi ya Lemonnier, FOS, CSL, na vituo vingine vya nje. Ukubwa wa bara la Afrika na idadi isiyotosha ya wanajeshi wa Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika yanalazimisha kuwepo kwa mitambo ya C4S ambayo itakabiliana na uwezo wa kimkakati. Uhamishaji na uimarishaji wa mfumo wa mitambo ya C4S pamoja na nia zake za kimkakati na kuwa miundombinu imara na yenye kuendelezwa ni jambo ambalo litaendelea kuwa uwekekezaji wenyewe kupewa kipaumbele kwa Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika.

Nyenzo

Kiwango cha fedha za kugharimia mipango iliopo chini ya mamlaka ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani ambacho kinapatiwa kwa matumizi Afrika kimeongezeka tangu kuundwa kwa Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika, na sisi tunaendelea kuomba fedha ili kuturuhusu kuendesha mambo ya ulinzi ambayo yameelezewa na kupewa kipaumbele na rais. Nchi katika mipango yeetu ya AOR mionganoni mwa nchi fukara sana duniani. Majeshi yao mengi hayakupata mafunzo bora, hayana vifaa bora vya kijeshi, hayakutayarishwa vyema kwa misheni zake za msingi – kama vile ulinzi wa taifa lao au kushiriki kwao katika operesheni za kulinda amani. Misafara ya majeshi ya Marekani na ya Afrika pamoja na vifaa kwenda kukabiliana na vitisho vyenye kujitokeza, kuendesha shughuli za kujenga uwezo, na kukabiliana na maafa, inategemea sana uwezo wa jeshi la Marekani angani na baharini.

Kugharimia kikamilifu mipango yenye kudhaminiwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani ni muhimu katika kusaidia washirika wetu kudumisha ushwari ambao huleta maendeleo, wakati tunawasadidia kugeuza sekta zao za usalama. Mahitaji makuu ni kama ifuatavyo:

Kugharimia Mpango wa FMF

Kwa mwaka wa fedha 2011 mahitaji ya FMF kwa Afrika yanafikia kiasi cha dola \$38 milioni, ambapo dola \$14 milioni zitatumika nchini Tunisia na Morocco. Kama tunataka kufanikisha malengo yetu ya kimkakati na kuzuia athari za muda mrefu, ni lazima tutowe fedha zenye kuhitajika kwa ukamilifu kwa ajili ya FMF kwa bara la Afrika. FMF ni muhimu katika kutekeleza misheni ya Marekani katika Afrika na ni uwekezaji wa muda mrefu ambao ni muhimu katika uhusiano. Kutolewa kwa fedha zisizotosha kugharimia mipango yetu ya FMF au ugawaji wa mwaka kwa mwaka usioridhisha unaweza kuharibu juhud zetu, na kuwafanya washirika wetu kugeukia nyanzo nyingine, na kuzuia shughuli za operesheni za kulinda amani. FMF ni muhimu kwa mkakati wetu wa kuzuia badala ya kukabiliana yanapotokea.

Kugharimia Mazoezi

Sehemu muhimu ya ujenzi wetu wa uwezo ni mpango wetu wa mazoezi ya pamoja ya kijeshi. Mpango huu unaendeshwa chini ya mpango wa mazoezi wa CJCS, na unategemea fedha kutoka mfuko wa mazoezi wa kamanda, uendeshaji na mafunzo (CE2T2). Wakati mamlaka hayo yanazidi kukuwa na kuimarika na mpango wetu wa mazoezi ukizidi kupanuka ili kukabiliana na mahitaji ya kuwa na majeshi yaliyotayari ya Marekani na majeshi ya washirika wetu, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kitatowa maombi yenye kuongezeka kwa ajili ya mazoezi hayo ya pamoja – CE2T2. Tunaomba uungaji wenu mkono wenye kuendelea kwa ombi lililotolewa na Wizara kwa ajili ya mfuko wa mazoezi wa kamanda, uendeshaji na mafunzo.

Kugharimia Juhudi za Kupambana na Biashara haramu ya Dawa za Kulevyta

Mapato yenye kutokana na uuzaaji wa dawa haramu za kulevyta ambazo zinasafirishwa kuititia Afrika moja kwa moja zinawanufaisha matajiri wa dawa za kulevyta ambao wanasantaza dawa za kulevyta katika mitaa ya Marekani. Ushawishi wa fedha zenye kutokana na dawa za kulevyta katika nchi zinazoendelea husababisha ulaji rushwa na kuathiri ushwari katika taifa, hali ambayo inaweza kutishia kupatikana kwa rasilimali muhimu kwa taifa la Marekani na kwa uchumi wa dunia mzima. Kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevyta zenye kuititia Afrika ni swala nyeti na muhimu kwa usalama wa taifa la Marekani, na sisi tunawasihi mufikirie kuunga mkono kikamilifu mpango huu.

Ushirikishaji wa Idara Mbalimbali na Michango

Ubunifu wa shughuli za Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika unategemea wazo la kwamba ushirikiano wa idara mbali mbali unasababisha upangaji bora na umoja mkubwa wa juhudini kutoka kwa washirika wote wa serekali ya Marekani. Kama ilivyoelezewa katika ripoti hii, maslahi ya taifa letu yamenufaika kutokana na hatua za Kikosi Maalulmu cha Jeshi la Marekani Afrika kushirikiana na idara mbali mbali. Juhudi zetu za pamoja zimesababisha matokeo yenye faida sana katika upande wa mabadiliko katika sekta ya usalama, ujuzi na utalaamu wa majeshi, ulinzi wa amani, misaada ya kibinadamu, matayarisho dhidi ya maafa, hatua za mipango ya kukabiliana na magonjwa ya halaiki, mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya, na mapambano dhidi ya ugaidi.

Changamoto za kuwaweka maafisa wa idara mbali mbali katika Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika zilitambulishwa hivi karibuni kuitia utafiti kabambe wa ndani. Matokeo yake ni kwamba, juhudini zinatekelezewa za kukabiliana na maswala ya mafunzo, upangaji wa mazoezi ya pamoja ya kijeshi, na elimu kwa wafanyakazi wa Wizara ya Ulinzi kuhusu uwezo wa idara mbali mbali. Sisi tunaelewa kwamba idara nyingine za serikali ya Marekani zina majukumu tofauti na malengo tofauti, na kwamba, ushirikiano na idara hizo ni wa njia mbili. Katika kila kitu ambacho tunakifanya, sisi tunataka kuhakikisha kwamba mipango na hatua za Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika inaunga mkono sera za Marekani Afrika. Sisi tunaendelea kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha kwamba kushiriki kwa idara mbali mbali za Marekani na Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika ni kwa manufaa ya washiriki wote, na hasa, kwa maslahi ya taifa letu.

Kuungeza fedha za kugharimia mipango inayohusu ulinzi ni jambo ambalo linapaswa kufuatana na utowaji wa juhudini sambamba na mipango ya kidiplomasia na maendeleo. Ugharimiaji wa kutosha wa mpango wa TSCTP unawezesha juhudini za idara za kiraia kuweza kuwasaidia washirika wetu katika kujenga na kudumisha hali ya mapambano dhidi ya makundi yenye siasa kali yenye kutumia nguvu. Tunalihimiza Bunge la Marekani liunge mkono juhudini za serikali ya Marekani kwa ujumla wake wakati linapokuja swala la diplomasia, maendeleo na ulinzi.

Mipango ya Kushughulikia Maslahi na hali za Wafanyakazi

Ofisi inayoshughulikia Hali bora za maisha (QoL) ya wafanyakazi, inahimiza ufikikaji, usawa, haki na hali bora ya maisha kwa kuitia huduma na mipango ya familia za Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika. Ili kutusaidia kutambuwa zingatio la hali bora za maisha, familia ya Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika katika bara la Afrika hushiriki katika mikutano ambayo hufanyika ili kukabiliana na changamoto zenye kutokana na familia ambazo zinaishi Afrika. Ili kusaidia timu yetu ya wafanyakazi na familia zao katika kutatuwa matatizo yenye kutokana na kuhamishwa pamoja na mabadiliko mengine ya familia, sisi tumetekeliza mpango wa ushauri kwa maisha ya wanajeshi na familia. Kuhusu swala la elimu, ushirikiano wetu na Shughuli za Elimu za Wizara ya Ulinzi ya Marekani pamoja na Shule za Jamaa wa Wanajeshi zenye kuendeshwa na Wizara ya Ulinzi katika Ulaya, ni hatua ambazo

zinaunga mkono elimu kwa wafanyakazi wote wa Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika. Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kitaendelea kuunga mkono na kupanuwa shughuli hizi katika mwaka wa fedha wa 2011.

Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kitaendelea kutathimini mazingira yote ili kutambuwa maswala yasiyo ya kawaida yenyeye kujitokeza katika swala zima la hali bora za maisha. Tutaimarisha uhusiano wetu wa kimkakati na washirika wetu ili kuleta maendesho bora na kushirikisha utatuzi ili kupunguza au kutatuwa hali za maisha. Tunaendelea kuzingatia juhudzi zetu kuwasaidia wafanyakazi na familia zao, waliopo katika bara la Afrika au nje ya bara hilo, ili kuhakikisha kwamba hali ya maisha yao inabakia kupewa kipaumbele na kugharimiwa inavyofaa.

HITIMISHO

Kipaumbele cha Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika ni kuendesha mipango yenyeye ufanisi ya ushirikiano katika swala la usalama wa kudumu na ushirikiano wa kijeshi ili kuendeleza na kulinda maslahi ya Marekani katika bara la Afrika. Mipango yetu inawasaidia washirika wetu wa Afrika kutekeleza majukumu yeye kuongezeka katika kukabiliana na wasi wasi wa ulinzi wa bara hilo na visiwa vyake. Kwa kuzingatia ujenzi uwezo wa muda mrefu, sisi tunatekeleza mkakati wa kuzuia ambao unatekeleza maslahi ya Marekani, washirika wetu wa Afrika, na washirika wetu wengine.

Marekani inafanikisha kwa ufanisi mkubwa shughuli zake wakati inaposhirikisha kazi zake na idara nyingine za serikali ya Marekani katika kutumia diplomasia, maendeleo na ulinzi ili kutimiza malengo yetu ya taifa. Bunge linaweza kuboresha mtazamo wetu wa taifa kwa changamoto zenyeye kutokeza ambazo zimethibitika katika miaka kumi ya kwanza ya karne hii mpya kwa kuunga mkono ugharimiaji kifedha na maendeleo ya idara na wizara nyingine za serikali ya Marekani ambazo zinashirikiana na sisi na kutuunga mkono. Katika kutathimini msaada wa usalama, mamlaka itaruhusu idara zote za serikali ambazo zinachangia katika sera zetu za nchi za nje na juhudzi za usalama wa taifa kuimarisha juhudzi zetu za umoja, na hivyo kuhakikisha kwamba tunakabiliana na vitisho vya kimataifa ambavyo havina kikomo kisheria.

Mimi nashukuru mno kwa uungaji mkono wa bunge la Marekani kwa Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika. Kuendelea kwenu kuunga mkono na upendo kwa wanaume na wanawake kutoka Wizara ya Ulinzi na idara na wizara nyingine za serikali ya Marekani ambao wanafanya kazi katika Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika kutaruhusu kazi zao bora za kulinda na kuendeleza maslahi ya Marekani. Mimi ninajivuna sana kwa kazi yangu katika Kikosi hicho Maalumu cha Jeshi la Marekani Afrika pamoja na Wamarekani hawa wenye bidii kubwa.

